JACKPOT BABA LAO!
TZS. 518,627,720
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Ofisa** Ustawi Jamii jela miaka 30 kunajisi mtoto

UKURASA 3


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Kasi ndoa za jinsia moja ni kuiandaa dunia kuwa 'jangwa'
TEKNOLOJIA
NA GAUDENSIA MNGUMI
MIAKA 2 YA MAMA
Tanzania inapong'ara kilimo, chakula Afrika
•Wasomi, wataalamu SIDO, SUA, NYUMBU wawe namba 1

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Machi 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581256

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


## MIAKA 2 YA SAMIA

# CHADEMA, ACT watoa ya moyoni

UKURASA 2

UKURASA WA 3

### TANZANIA YAISAIDIA MALAWI BIL. 2/- ATHARI ZA KIMBUNGA



SERIKALI ya Tanzania imetuma helikopta mbili nchini Malawi zenye msaada wa vifaa, chakula pamoja fedha Dola milioni moja..

UKURASA WA 4

### NDEGE YA MIZIGO ATCL KUWEKA HISTORIA SADC

UJIO wa ndege ya kwanza ya mizigo ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) Boeing 767-300F unatarajiwa kuweka historia kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC)...

UKURASA WA 19

### MAANDAMANO YARINDIMA KENYA, AFRIKA KUSINI

MAANDAMANO yameshuhudiwa nchini Kenya na Afrika Kusini, huku polisi wa mataifa yote mawili wakifanya jitihada mbalimbali kuyazuia ikiwamo kurusha mabomu..

### Samia aonya watakaochezea fedha miradi 'Better tomorrow'

UKURASA 2



Vijana 812 kutoka mikoa mbalimbali nchini wakimsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) kwenye uzinduzi wa programu ya Kilimo cha Mashamba Makubwa ya Pamoja (Block Farming) Chinangali mkoani Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Askari anayetuhumiwa kuingiliwa kinyume maumbile asomewa mashtaka

UKURASA 3

MICHEZO **MAYELE NI SHIDA YANGA - MONASTIR** UK.24

MAONI UK.6



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati), akiangalia jambo kuhusu miundombinu ya jengo la ubalozi kwenye simu ya Mwambata wa Kijeshi, Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza, Brigedia Jenerali Bright Msuya (kushoto). Kulia ni Balozi wa Tanzania, Uingereza Dk. Asha Rose Migiro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA, ACT watoa ya moyoni maadhimisho UWT

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), vimesema siri ya wao kushiriki katika maadhimisho ya miaka miwili ya utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan yaliyoandaliwa na Chama cha Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) ni maridhiano yanayoonyeshwa na kiongozi huyo.

Wakitoa maoni yao kuhusu mkutano huo, wachambuzi wa siasa wamesema kuwa kujumuika kwa pamoja kwa wanasiasa hao ni jambo jema ambalo linawaweka watu pamoja, kuliko kuishi kwenye chuki na uhasama.

Katika maadhimisho hayo yaliyofanyika juzi washiriki walikuwa kutoka vyama mbalimbali vya siasa walialikwa wakiwamo wa Chama cha ACT-Wazalendo na CHADEMA.

Akizungumza na Nipashe kuhusu ushiriki wa wanawake wa chama chao katika maadhimisho hayo, Katibu Mkuu ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema walifanya hivyo kwa kuzingatia mambo matatu.

Alisema moja ya sababu zilizowasukuma kuruhusu wanawake wa chama chao kushiriki ni kutokana na siasa za maridhiano zinazoonyeshwa na Rais Samia.

Sababu nyingine alisema ni kumpa moyo Rais Samia katika ahadi yake aliyoitoa ya Katiba mpya, Tume huru ya uchaguzi na mageuzi ya kisiasa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Ado, alisema ya tatu ni kuonyesha ushiriki wao katika msukumo wa ajenda ya mwanamke katika kupambana dhidi ya vikwazo vyote ambayo vinawakumba wanawake nchini.

"Sisi tumeshiriki tukio la kilele cha maadhimisho ya miaka miwili ya Rais Samia madarakani kwa sababu ya siasa za maridhiano ambazo amezikubali kuwa ndizo zinazoongoza duru za kisiasa hivi sasa na zinabadilisha pia mahusiano baina ya vyama," alisema Ado.

"Tunaona Rais Samia mwenyewe anashiriki shughuli za vyama. Kwa mfano hivi karibuni alishiriki tukio la BAWACHA, hiyo inaongeza chachu kwa vyama kuendelea kushirikiana kwenye matukio. Haina maana kwamba tunaunga mkono lengo la tukio husika ila tunakwenda kuonyesha mshikamano na maridhiano ya kisiasa.

"Lakini tunashiriki katika matukio haya kumpa moyo Rais juu ya ahadi yake aliyoitoa ya Katiba mpya, Tume Huru ya Uchaguzi na mageuzi ya kisiasa kwa ujumla wake. Tunamwonyesha kwamba tuko pamoja kwenye hilo na tutashirikiana kujenga Tanzania mpya, kufungua ukurasa mpya.

"Na tuliwaruhusu wanawake ili kuonyesha ushiriki wetu katika msukumo wa ajenda ya mwanamke katika kupambana dhidi ya vikwazo vyote, ambayo vinawakumba wanawake na kuonyesha kwamba tuko tayari kushirikiana nje ya vyama vya siasa kwa ajili ya mustakabali mwema wa mwanamke wa ushirikishwaji na kuinuliwa kwao kisiasa, kiuchumi na kijamii."

Kaimu Mwenyekiti wa BAWACHA, Sharifa Suleiman, alisema suala la vyama vya siasa kualikana kwenye matukio ni jambo la kawaida kwa ujenzi wa demokrasia.

"Sisi BAWACHA tulimwalika Rais wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake tuliyoiandaa na kuhudhuria. Kwa hiyo, kualikwa kwetu ni matokeo ya maadhimisho hayo. Ni jambo jema kualikana kwasababu sisi kama chama cha siasa hatuna ugomvi na chama tawala na vyama vyingine kwa sababu CHADEMA tuna dhamira ya kuliongoza taifa bila ubaguzi," alisema.

"Lakini kimsingi hali hii imetokana na kufunguliwa kwa ukurasa mpya wa siasa kwa vyama vyetu kupitia maendeleo ya mazungumzo ya maridhiano yanayoendelea baina ya chama chetu na serikali kwa pamoja na chama kinachoongoza serikali yaani CCM.

"Kwa kifupi siri ya mafanikio haya ni mazungumzo ya maridhiano baina ya vyama vyetu na serikali inayoongozwa na Rais Samia na Makamu Mwenyekiti wa CCM, Abdulrahman. Kinana kwa upande mmoja na Mwenyekiti wetu wa chama chetu taifa, Freeman Mbowe."

Mjumbe wa kikosi kazi ngome ya ACT-Wazalendo Taifa, Halima Ibrahim Mohammed, alisema jambo kubwa lililowasukuma wao kushiriki ni namna wanavyoona mabadiliko anayoyaleta Rais Samia hususani katika kuonyesha kwamba siasa si uhasama.

"Tumeona mabadiliko kwa Rais Samia, hakuna jambo zuri kama nchi kuwa na amani, anaweka mazingira ya siasa yasiwe ya uhasama, chuki. Hilo ni jambo jema kwa sababu hii nchi ni yetu sote," alisema.

Naye mchambuzi wa masuala ya siasa, Nassoro Kitunda, alisema kilichofanyika juzi kwa wanawake kukutana bila kuangalia vyama vyao vya siasa ni jambo jema na ndivyo inatakiwa kuwa badala ya kuwekeana chuki.

Pia alisema anaamini kwamba hali hiyo imetokana na utayari wa Rais Samia wa kutaka maridhiano.

"Tulikuwa tunahitaji kuwa na siasa za namna hii. Siasa za kukaa pamoja na kuzungumza masuala na siyo kukashifiana au kurushiana lugha zisizo na staha. Tunahitaji siasa za kushindana kwa hoja na ushawishi, kwa hiyo kilichofanyika katika tukio la jana (juzi) kwa wanawake kutoka vyama mbalimbali vya siasa kukaa pamoja ni jambo jema sana,"alisema.

"Hatusemi kwamba siasa za namna hiyo zimeisha, lakini hata huu mwanzo ni mwema na hali hii imetokana na Rais Samia mwenyewe kuonyesha nia hiyo na kuwachukulia vyama vingine kwamba sio wapinzani bali ni vya kusaidia katika kuibua hoja na ndio maana hata wao wapinzani wamepata amani kushiriki."

Alisema ni vema maridhiano yanayofanywa kwa vyama vya siasa na serikali yakafanywa pia na kwa wananchi kwa kuhakikisha wanasikilizwa na kutatuliwa changamoto zote zinazowasumbua.

# Rais Samia aonya watakaochezea fedha miradi 'Better tomorrow'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewaonya watendaji watakaojaribu kuchezea fedha zilizowekezwa kwenye mradi wa mashamba makubwa ya pamoja kwa Watanzania.

Amesema mradi huo utaifikisha nchi kwenye uwezo wa nchi kujitosheleza kwa chakula na kuilisha dunia.

Alitoa onyo hilo jana baada ya kuzindua mradi huo uliopo kupitia Programu ya Building Better Tomorrow (BBT) eneo la Chinangali, mkoani hapo.

Rais Samia alisema, programu hiyo ni mwanzo wa safari ya kufikia mwaka 2030 kilimo cha mazao kwenye pato la taifa kiwe asilimia 10 kutoka 3.6.

"Sitavumilia Bashe (Waziri wa Kilimo Hussein Bashe) na wenzio nimetoa fedha za wavuja jasho Watanzania ziende kwenye matumizi ya kilimo zikazalishe, sitaki fedha zichezewe, sitavumilia."

Rais Samia alisema kila walichohitaji wamepewa kama kushindwa watashindwa wao kwa kutokuwa na dhamira na hatua hiyo ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM.

"Suala hili ni la kitaifa sio la kilimo peke yake, nendeni mkaunde kamati ya mawaziri watakaoshughulikia jambo hili, sitaki kusikia tumeshindwa, hakuna kushindwa lazima twende na tufanikiwe," alisema.

Alisema mpango huo ulipotangazwa vijana zaidi ya 20,000 walijitokeza na kuwataka waliopata fursa hiyo kufanya kazi iliyokusudiwa na serikali itakuwa nao na yote waliyoahidiwa watapatiwa ili wazalishe mazao ya chakula na biashara.

"Tutaendelea kutenga bajeti mahsusi kwa ajili ya kuajiri watumishi wa sekta ya umwagiliaji, tumeajiri hawa 300 tutaendelea kutoa ajira ili vijana wawe wengi sehemu zote kuwe na vijana wanaokwenda sekta ya kilimo," alisema.

Alitoa rai kwa wadau wa kilimo kushirikiana na Wizara ya Kilimo na kuwataka makandarasi wazawa kuhakikisha kazi walizopewa wanazifanya kwa uaminifu na kiwango kinachotakiwa.

"Mmesaini mikataba leo ombi langu makandarasi wa ndani kazi hizi zimetolewa kwenu lazima mwoneshe uwezo," alisema.

Naye Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema kutakuwa na vituo atamizi vya vijana wa kilimo 13 ambao watapata malazi, chakula na mafunzo huku vijana 812 wanatarajiwa kuanza mradi wa BBT watakaopata hekari 10 kila mmoja.

"Vijana watafundishwa kuhusu kilimo chenyewe tuna wahitimu wa vyuo mbalimbali na jambo ambalo sisi limetushtua ambalo pia ni faraja katika vijana tuliowapokea kinadada 10 ambao wamejifungua wana watoto wa mwezi mmoja na miwili tuliwashauri warudi kulea watoto nyumbani ndio waje, wakakataa sasa tutawaweka kwenye maeneo maalum kuna mwingine amekuja na mume wake amlelee mtoto," alisema.

Aidha, Bashe alisema takwimu zimekuwa zikionesha Tanzania ina hekari 712,000 za umwagiliaji, lakini ukweli kuna mifereji hakuna skimu za umwagiliaji na kwa sasa zinafanyiwa maboresho.

Alisema miundombinu ya mashamba hayo itajengwa kwa miaka miwili hadi mitatu, huku akiwatoa hofu Watanzania kuhusu mashamba makubwa na kwamba serikali imeamua kuwakomboa vijana kupitia kilimo.

"Usingechukua hii hatua Rais Samia kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa shamba la zabibu la hekari moja kuweka miundombinu inagharimu Sh. milioni 10, vijana hawa watapewa mafunzo kwa miezi minne na baada ya hapo watapelekwa shambani na kukabidhiwa hati ya umiliki wa ardhi ya miaka 99," alisema.

Alisisitiza Wizara ya Kilimo haitatoa hata shilingi moja ya umwagiliaji kwenye eneo ambalo halina mfumo mzuri.

Bashe alisema kilimo sio kubeti bali ni mpango wa muda mrefu, vijana hao wamepata fursa ya kumiliki ardhi hekari 10, wamesafishiwa kwa Sh. milioni 1.8 kwa hekari, wamewekewa miundombinu na kuwapandia.

Alisisitiza hadi kufikia mwakani maofisa kilimo watakuwa na vitendea kazi vya magari.

Pia aliomba sekta binafsi kushirikiana na serikali kwenye uwekezaji wa sekta hiyo kwa kuwa hadi sasa wameomba watatu ardhi ya uwekezaji.

Naye Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema mashamba hayo yanahitaji ushirikiano wa wizara zote ili kutimiza azma ya kuilisha dunia kwa kuwa Tanzania ina uwezo huo.

Awali Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, David Kihenzile, alisema Rais Samia ametafsiri ndoto ya kilimo kuwa ya vitendo na inaajiri asilimia 70 ya Watanzania.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (wa pili kushoto), Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano WCF, Laura Kunenge, wakijadiliana jambo wakati wa kikao kazi kilichoandaliwa na WCF kuwapa elimu ya fidia wanachama wa TEF, Bagamoyo mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ofisa Ustawi Jamii jela miaka 30 kunajisi mtoto

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

OFISA Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Frank Mabuga, amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela, baada ya kukutwa na hatia ya kumnajisi mtoto mwenye umri wa miaka 13.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi Mahakama ya Wilaya ya Kigoma, Eva Mushi, baada ya kusikiliza mashahidi wa pande zote mbili.

Alisema mahakama ilisikiliza mashahidi sita wa upande wa mashtaka na ilikuwa na vielelezo viwili vya PF3 pamoja na ramani ya eneo la tukio.

Wakili wa mshtakiwa huyo, Ignatus Kagashe, aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa ana mtoto mdogo na mzazi mwenzie ni mjamzito.

Wakili wa Serikali, Happiness Mayunga, alidai mahakamani kuwa mtuhumiwa alishindwa kusimamia dhamana aliyopewa ya kulinda haki ya mtoto kupitia cheo cha Ofisa Ustawi wa Jamii na kuamua kwenda kinyume na taratibu kwa kufanya kitendo hicho, ni haki kwa mahakama kutoa hukumu.

"Kitendo cha mtuhumiwa kufungwa miaka 30 jela ni tafsiri kwamba haki imetendeka," alidai wakili huyo akizungumza na waandishi wa habari nje ya mahakama.

Aidha, aliiomba jamii kumlinda mtoto na kukemea vitendo vyovyote vya ukatili vinavyofanyika dhidi yake.

Frank alipandishwa mahakamani Februari 22, mwaka jana, akidaiwa kumwingilia mtoto huyo mara mbili katika nyumba ya kulala wageni.

# Askari anayetuhumiwa kuingiliwa kinyume na maumbile asomewa mashtaka mahakamani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ALIYEKUWA Askari Polisi FFU, Ramadhani Hassan Ali maarufu Afande Rama, amefikishwa katika Mahakama ya Mkoa wa Vuga, kujibu mashtaka mawili yanayomkabili.

Mbele ya Hakimu Khamis Ali Simai, Mwendesha Mashtaka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Muhammed Saleh, alidai mahakamani kuwa mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka mawili ambayo ni kuruhusu kuingiliwa kinyume na maumbile na kufanya maudhui makubwa ya kingono.

Alidai kuwa mshtakiwa alitenda makosa hayo mapema Machi mwaka huu, kitendo ambacho ni kosa kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar.

Mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza akitokea mahabusu ya polisi bila ya wakili wa kumsimamia.

Shtaka hilo limeahirishwa hadi Aprili 4, mwaka huu na mshtakiwa amepelekwa mahabusu huku upande wa mashtaka ukidai unaendelea na upelelezi.

Ilidaiwa kuwa askari huyo alijihusisha na mapenzi ya jinsia moja kwa kuruhusu kuingiliwa kinyume na maumbile huku video fupi inayoonesha tukio hilo ikisambaa mtandaoni.

Hivi karibuni, Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, alisema askari huyo alishapandishwa kwenye mahakama ya kijeshi kutokana na tuhuma hizo ambazo ni kinyume na mwongozo na kanuni za kiutendaji wa jeshi hilo (PGO).

# Tanzania yaisaidia Malawi bil. 2/- athari za kimbunga

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Tanzania imetuma helikopta mbili nchini Malawi zenye msaada wa vifaa, chakula pamoja fedha Dola milioni moja (Sh. bil. 2.3) taslimu kwa ajili ya kusaidia walioathiriwa na kimbunga Freddy, nchini humo.

Kwa mujibu wa chanzo cha kuaminika kilichoifikia Nipashe jana, Tanzania imetuma msaada wa kibinadamu, pamoja na helikopta mbili za kijeshi zitakazosaidia shughuli mbalimbali.

Msaada huo ni pamoja na tani 1,000 za chakula, blanketi 6,000 na mahema 50.

Msemaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Gaudentius Ilonda, alisema: "Helikopta mbili zimeruka kutoka Dar es Salaam kwenda Malawi kusaidia shughuli za uokoaji katika maafa yanayoendelea.

"Pia serikali imetoa vifaa kama blanketi na mahema na shehena za chakula zitapelekwa kila siku mpaka kufukia tani 1000," alisema.

Balozi wa Tanzania nchini Malawi, Humphrey Polepole, alithibitisha kupokewa kwa msaada huo na kwamba Serikali ya Tanzania, itaendelea kusaidia nchi hiyo katika kipindi hiki kigumu.

"Katika kuhakikisha ndugu zetu wa Malawi wako salama na kuvuka kipindi hiki vizuri, Serikali ya Tanzania imetoa msaada ukiwamo wa fedha taslimu Dola milioni moja, chakula na vifaa vingine, " alisema Polepole.

Tanzania inapakana na Malawi, upande wa Kusini na imekuwa na mwingiliano mkubwa wa watu.

Malawi, Madagascar na Msumbiji zimekumbwa na madhara ya kimbunga Freddy. Zaidi ya watu 400 waliuawa na maelfu ya nyumba kuharibiwa.

Eneo la Kusini mwa Afrika, mara nyingi hukumbwa na vimbunga na dhoruba za kitropiki zinazoingia kutoka Bahari ya Hindi.


**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)**

**UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA AJIRA ZA MUDA KWA KAYA ZA WALENGWA**

Miradi ya ajira ya muda kwa walengwa wa TASAF ni utaratibu wa utekelezaji miradi ya jamii yenye kutumia nguvu kazi, inayoshirikisha walengwa kufanya kazi na kulipwa ujira. Miradi hiyo inawezesha jamii kupata rasilmali /miundombinu inayotoa huduma na ujuzi kwa jamii kupitia ushiriki wao katika kutekeleza miradi hiyo.

Washiriki wa kazi zinazotoa ajira ya muda kwa walengwa ni watu wenye uwezo wa kufanya kazi wenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 65. Kila kaya ambayo inashiriki katika ajira za muda kwa walengwa inaandikisha watu wawili, ambapo mtu mmoja kutoka kwenye kaya ndiye atashiriki kazi kwa wakati mmoja. Utekelezaji wa miradi ya ajira ya muda huchukua miezi sita ambapo walengwa hufanya kazi kwa siku kumi tu kwa kila mwezi. Kwa siku mlengwa anatakiwa kufanya kazi kwa muda usiozidi masaa manne ili aweze kupata muda wa kufanya shughuli nyingine.

Wazee, watu wenye ulemavu, wakina mama wajawazito na wenye watoto wadogo ambao hawajatimiza miaka miwili hawaruhusiwi kufanya kazi za ajira za muda kwa walengwa. Wasimamizi wanaopanga kazi za walengwa hawatakiwi kuwapangia kazi watu hao na wanapaswa kutoa taarifa kwa wajumbe wa kamati ya usimamizi wa mradi (CMC) na Waratibu ili majina ya watu hao yaondolewe kwenye orodha ya watu walioandikishwa kufanya kazi za ajira ya muda. Kaya yenye watu ambao hawaruhusiwi kufanya kazi za ajira ya muda watapokea ruzuku ya msingi.

Uongozi wa TASAF umetoa waraka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Ufuatiliaji kupitia orodha za watu walioandikishwa kufanya kazi kwenye miradi ya ajira za muda na kuwaondoa wale ambao hawaruhusiwi kufanya kazi kwenye miradi hiyo. Aidha utoaji wa elimu kwa viongozi wa jamii, wasimamizi na walengwa kuhusu taratibu za utekelezaji wa miradi ya ajira za muda kwa kaya za walengwa utaendelea kutolewa katika kipindi chote cha utekelezaji.

**Imetolewa na**

**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**
**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TASAF**

217333102

# Mvua yaacha kilio Kariakoo

**Na Jenifer Gilla**

NI hasara. Ndivyo wanavyosema wafanyabiashara wa Mtaa wa Nyamwezi, Kariakoo jijini Dar es Salaam, baada ya mvua iliyonyesha juzi kuingia ndani ya maduka yao kulowesha bidhaa na kuziathiri.

Wamesema hali hiyo imesababishwa na mitaro inayopitisha maji ya mvua kuziba na kufurika kukosa sehemu ya kwenda na kuingia ndani ya maduka hayo.

Wafanyabiashara hao wameiomba Manispaa ya Ilala kuiboresha mitaro hiyo ili kuzuia tatizo hilo kujirudia kutokana na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), kutabiri kuendelea kunyesha kwa mvua.

Baadhi ya maduka yaliyotembelewa na mwandishi wa habari hizi, yalikutwa wafanyabiashara wakitoa maji kwenye maeneo yao na wengine wakichambua nguo zilizolowa na maji na kuzifunga kwenye viroba kuzipeleka nyumbani mwao kuzianika.

Mmoja wa wafanyabiashara waliopata adha hiyo, Nassoro Samata, alisema hasara aliyoipata ni kubwa kutokana na mzigo mpya aliokuwa anategemea kuuza jana kulowa na maji ya mvua hali inayomlazimu kuzianika kabla ya kuziuza. "Mzigo ndio nimeushusha juzi Jumamosi, nikauweka hapo kwa ajili ya kuanza kuuza leo (jana), kama unavyouona asilimia kubwa umelowa, kwa kuwa umeshaingia maji ukikauka unakuwa hauna upya tena sio rahisi mteja kuvutiwa nao," alisema Nasoro.

Alisema kwa makadirio amepata hasara ya karibuni milioni 15, kwa kuwa atalazimika kuuza bei ya hasara, ili uishe baada ya maji kusababisha thamani ya bidhaa hiyo kushuka.

Naye mfanyabiashara wa suruali za jinzi, Furaha Chasu, alisema karibu ya nusu ya bidhaa zilizokuwa dukani zimelowa kwa sababu hakuwahi kuziondoa kama walivyofanya wengine kwa kuwa anaishi mbali na eneo hilo. Alisema alipigiwa simu na majirani zake waliofungua biashara siku hiyo na kumtaarifu kuwa maji yameingia kwenye duka lake, lakini ilimchukua saa tatu kufika eneo la tukio na kukuta nguo nyingi zimeshalowa.

"Hasara ni kubwa hapa siwezi kusema, mpaka nikae chini nihesabu nguo zote zilizolowa, nitenge zipi zinafaa kuuza na zipi hazifai ndio nitajua hasara, nguo nyingi nilizokuwa nimepanga chini zimelowa na maji," alisema.

Naye Nancy Alfred, mfanyabiashara wa nguo za ndani za kike alisema bado anafikiria kama azitupe au aziuze kwa bei ya hasara kwa kuwa zimeshatoka kwenye hali ya upya sio rahisi kupata wateja. "Mteja ameshazoea huku kunauzwa nguo mpya, unapoweka nguo iliyoingia maji hasa hizi za ndani, anapata mashaka, ukizingatia haya maji ni ya kwenye mitaro sio salama, kwa kweli nimepata hasara kubwa," alisema huku akibubujikwa na machozi.

Aidha, mfanyabiashara Gloria Tarimo alisema hali hiyo imemshtua kwa kuwa ndio mara ya kwanza jengo hilo kuingiliwa na maji na kuiomba manispaa kuirekebisha mitaro hiyo haraka ili isijirudie tena.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imefanya utabiri wa hali ya hewa kwa mwezi Februari na Machi mwaka huu, ikitarajiwa kuwa na vipindi vya mvua kwa baadhi ya mikoa ikiwamo Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa katika tovuti ya mamlaka hiyo imeonyesha mikoa mingine itakayokuwa na hali hiyo ni Tanga, Kaskazini mwa Morogoro, Pwani na visiwa vya Unguja na Pemba, Kigoma, Katavi, Tabora, Dodoma, Singida, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa, Mtwara, Lindi na Ruvuma.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Amani Mafuru, aliwatupia lawama baadhi ya wafanyabiashara kwamba wamekuwa wakitupa taka katika mitaro hiyo, ikiwamo vipande vya nguo hali inayosababisha kuziba na kuleta majanga kama hayo mvua zinaponyesha.

"Kwenye kampeni zetu ya safisha pendezesha jiji, tunawatembelea na kuhamasisha usafi wa hasa mitaroni kila mara, lakini wengine hawatokei na wengine hurudia kutupa taka hizo kwenye mitaro ambayo tumeishaisafisha," alisema.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara hao kuacha kutupa taka kwenye mitaro hiyo na wakazi wa maeneo hayo waliounganisha chemba za maji taka kuwa ndio vyanzo vikuu vya kuziba na kuwasababishia usumbufu.

# Mabaharia wanolewa kuzalisha wanafunzi wenye sifa kimataifa

**Na Restuta James**

MABAHARIA wakufunzi na wahadhiri wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), wameanza mafunzo ya kuwajengea uwezo ili waweze kuandaa wanafunzi wenye sifa za kimataifa.

Akifungua mafunzo hayo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Msaidizi Usalama na Mazingira katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Injinia Michael Magesa, alisema mafunzo hayo yanayotolewa na Shirika la Bahari Duniani (IMO), ni muhimu kwa ajili ya kuzalisha wataalamu hao wenye uthibitisho wa kimataifa.

Alisema mafunzo ya ubaharia yanazingatia viwango vya IMO kutokana na utendaji wake kuhusu nchi mbalimbali duniani.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Kaimu Mkeyenge, alisema lengo la mafunzo hayo ni kukuza kiwango cha elimu kwa mahabaria wa Tanzania ili kukuza fursa ya ajira zao duniani.

Alisema mafunzo hayo yatatolewa kwa siku tano kwa washiriki 35 wakiwamo wakufunzi, watumishi wa TASAC na wajumbe wa bodi ya usahihishaji wa mitihani ya bahari.

Naye Kaimu Mkuu wa Chuo DMI, Dk. Tumaini Gurumo, alisema washiriki wa mafunzo hayo watajifunza namna ya kuandaa masomo kwa kuzingatia mkataba wa kimataifa na miongozo ya elimu na mafunzo kwa mabaharia unaosimamiwa na DMI.

Alisema baada ya mafunzo washiriki watapewa vyeti na IMO itakuwa inafanya ukaguzi baada ya miaka mitano, ili kuona kama chuo kinatoa mafunzo kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

"Miongozo ya kimataifa inatoa maelekezo ya sifa za wanaowafundisha hawa mabaharia, namna ya kuandaa somo, ufundishaji na namna ya kutunga mitihani...tuliomba haya mafunzo, ili tuendelee kuwa katika viwango vya kimataifa," alisema.

Alisema mafunzo hayo yatapanua wigo wa ajira kimataifa na kutoa wito kwa vijana kujiunga na chuo cha bahari kwa kuwa fursa za ajira ni nyingi.

# Ndege ya mizigo ATCL kuweka historia SADC

**Na Joseph Mwendapole**

UJIO wa ndege ya kwanza ya mizigo ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) Boeing 767-300F unatarajiwa kuweka historia kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Hayo yalisemwa jana na Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, wakati akifungua mkutano wa mwaka 2022/23 wa wadau wa usafirishaji mizigo, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Katika mkutano huo uliohusisha wafanyabiashara pamoja na wawakilishi kutoka taasisi mbalimbali za serikali, Mchechu alisema ATCL inatarajia kupokea ndege ya kwanza ya mizigo aina ya Boeing 767-300F yenye uwezo wa kubeba tani 54 mapema mwezi Aprili, 2023 ambayo itatatua changamoto ya usafirishaji mizigo ndani na nje ya nchi.

Awali ATCL ilikuwa ikitumia ndege za abiria kusafirisha mizigo ambazo zilikuwa na uwezo wa kubeba tani chache kulinganisha na uhitaji halisi wa soko.

Mchechu aliitaka ATCL kuendesha biashara hiyo kiushindani ikiwamo kuimarisha ushirikiano na wadau wao ili kutatua changamoto zinazoweza kukwamisha ufanisi wa biashara hiyo na kusimamia maslahi ya pande zote, yaani wadau na serikali.

Alifafanua kwamba ofisi yake ina wajibu wa kusimamia mashirika yote nchini likiwamo ATCL ili kuhakikisha yanajiendesha kimkakati kupitia uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali.

Akitaja takwimu za mahitaji ya soko duniani, alisema kwa mujibu wa Ripoti ya Soko la Usafirishaji wa Mizigo ya 2023, ukubwa wa soko la mizigo limekua kutoka Dola bilioni 191.01 mwaka 2022 kufikia Dola bilioni 199.09 mwaka 2023 kwa kiwango cha ukuaji (CAGR) cha asilimia 4.2.

Alisema kiwango hicho ni kwa ukubwa wa soko la usambazaji wa mizigo unaotarajiwa kukua hadi Dola bilioni 224.78 mwaka 2027 kwa kiwango cha CAGR ya asilimia 3.1.

Pia alisema Tanzania inaingia rasmi kwenye historia ya biashara ya ndege ya mizigo ambayo sio tu kwa Afrika Mashariki bali hata kwa nchi za SADC.

"Hakika, serikali imewekeza ATCL sambamba na Mpango wa Taifa wa Maendeleo pamoja na Ilani ya Uchaguzi kwa lengo la kuwezesha ukuaji wa uchumi, kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji na biashara nchini ambapo biashara ya mizigo inakuwa kwa kasi duniani," alisisitiza.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, alisema tangu kuhuisha mpango wake wa biashara wa mwezi Oktoba 2016, ATCL inajivunia kwa kutoa huduma za uhakika, salama na endelevu za ubora wa juu duniani kote.

Kupitia mkutano huo wa wadau wa mizigo, ATCL itakusanya maoni sahihi kutoka chanzo halisi yatakayowezesha kuondoa kero na urasimu kwenye biashara ya mizigo.

"Yapo mambo yanayotakiwa kufanyiwa maboresho hasa yenye urasimu, lakini yapo ambayo ni ufuataji wa sheria za kulinda usalama wa uendeshaji wa biashara hii. Katika kikao hiki wadau watajadili na kukubaliana masuala ya kufanyiwa kazi na kuweka malengo. Lakini tutaambiana ukweli kwa wafanyabiashara ambao hawafuati sheria ambazo kimsingi ni kwa faida ya pande zote mbili," alisema.

ATCL ina ndege 12 na imefanikiwa kupanua mtandao wake hadi kufikia vituo 14 vya safari za kitaifa, nane za kikanda na mbili za mabara.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UGAVI WA VIFAA VYA UMEME VYA KUSIMIKA ARDHINI (EARTHING & GROUNDING MATERIALS)**

**KUMBUKUMBU NAMBA: ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0117**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwenye Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za awali za ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakilia katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa utoaji wa huduma za:

**- Ugavi wa Vifaa vya Umeme vya Kusimika ardhini.**

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**
**Earthing:** 50mm isolated cupper conductor
**Grounding:** 50mm cupper conductor

Vifaa vya Chapa ya **Hilti** au inayofanana.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:
- Profaili ya kampuni iliyo na uthibitisho wa rasilimali zenye uwezo kutekeleza kandarasi husika.
- Karatasi ya Data (datasheet) ya vifaa muhimu
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli za matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa nia, unapendekezwa sana.
- Uthibitisho wa usajili na leseni ya biashara kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa Usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania.
- Uthibitisho wa Hati Safi ya Mlipa Kodi ya mwaka uliopita, 2022.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz** (Ukubwa wa barua pepe na viambatanishi: **20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 4 Aprili 2023, 12:00 jioni Saa za Tanzania.**

**Kichwa cha ombi kijumuishe nambari ya kumbukumbu kama ilivyoonyeshwa kwenye kichwa cha tangazo hili la EOI.**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

## MATANGAZO

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF LINDI
*(AT LINDI)*

CRIMINAL CASE NO. 05 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

DAUD POYO……………………………………………………ACCUSED PERSON

**To:**
Daud Poyo
Kibutuka Village
Liwale District
Lindi

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 28TH day of APRIL 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 14TH day of MARCH 2023

…………………………………
RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE LINDI

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name……………………………………

Signature…………………………………

Qualification/Relationship
Date………………………………………

217333502

---

Mention - 22/03/2023

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF TANGA
*(AT TANGA)*

CRIMINAL CASE NO. 3 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

HUSNA ALLY HEMED

**To:**

Husna Ally Hemed
Plot No. 13, Block 104, Ngamiani Area
Tanga City Centre
**Tanga Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 22nd day of March 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 9th day of March 2023

…………………………………
RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Duplicate Served Upon Me:**

Name……………………………………

Signature…………………………………

Qualification/Relationship

Date………………………………………

217333502

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF LINDI
*(AT LINDI)*

CRIMINAL CASE NO. 06 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

LITO CHANDE KIGWAGILO……………………………………ACCUSED PERSON

**To:**
Lito Chande Kigwagilo
Lionja Village
Nachingwea District
Lindi Region

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 28 day of APRIL 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 14TH day of MARCH 2023

…………………………………
RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE LINDI

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name……………………………………

Signature…………………………………

Qualification/Relationship
Date………………………………………

217333502

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE DISTRICT MAGISTRATE'S COURT OF BABATI
*(AT BABATI)*

CRIMINAL CASE NO. 31 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

OIL & GAS LIMITED………………………………………………ACCUSED PERSON

**To:**
Managing Director
Oil & Gas Limited
Plot No. 71, Block P, Magugu,
**Babati District, Manyara Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 24th day of April 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 17th day of March 2023.

…………………………………
RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE BABATI DISTRICT COURT

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**
Name……………………………………

Signature…………………………………

Qualification/Relationship
Date………………………………………

217333502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mshikamano huleta maendeleo, mabadiliko

**WAKATI** Rais Samia Suluhu Hassan akitimiza kipindi cha miaka miwili tangu alipoapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Watanzania wana kila sababu ya kusherehekea mabadiliko aliyoyaleta nchini hasa katika kuhakikisha wananchi wake wanakuwa wamoja bila kujali itikadi zao za kisiasa, kidini, kikabila wala rangi.

Hili limejionesha wazi baada ya kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa ambayo ilikuwa imefungiwa sasa kuendelea kama kawaida, lakini kwa kuzingatia misingi ya sheria kwa kuepusha vurugu na lugha zisizofaa.

Hatua hiyo ya Rais Samia imeleta imani kwa wanasiasa waliokimbilia nje ya nchi kutafuta hifadhi na sasa kurudi nyumbani bila hofu yoyote.

Hivi ndivyo Rais Samia anavyotaka Tanzania anayoingoza iwe, lakini ni lazima apate ushirikiano kutoka kwa watu anaowaongoza.

Dalili nzuri za nchi kuwa na umoja zimeanza kujitokeza baada ya Rais Samia kuwa kiongozi wa kwanza wa chama tawala kushiriki katika kongomano la chama cha upinzani.

Na katika kuonesha mwendelezo wa mshikamano huo, juzi wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka miwili ya Rais madarakani, wanawake wa vyama vya upinzani walishiriki katika maadhimisho hayo yaliyoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) na kuonekana wakiwa na furaha ya kuketi pamoja.

Wakati akiwahutubia wanawake hao, Rais Samia aligusia suala la usawa wa kijinsia hasa kufikia 50/50 huku akibainisha kuwa kwenye nafasi ya mwanamke katika uongozi, kuna ongezeko la nafasi za wanawake kiuongozi na kutaja maeneo yenye viongozi wanawake kuwa ni pamoja na Mahakama Kuu, Maofisa Tawala wa mikoa na kusema bungeni bado kuna kazi ya kufanya.

Hata hivyo, aliwahakikishia wananchi kuwa huko nako wanakwenda pole pole ili hata isipofika asilimia 50 basi hata asilimia 40.

Kufikia asilimia hiyo sio jambo dogo, linahitaji ushirikiano wa hali ya juu kwa wanawake kuinuana na kuwezeshana, kupeana moyo na kujitokeza kugombea nafasi zinazotangazwa.

Hilo litawezekana kama wanawake wa vyama vyote vya siasa watashirikiana na kuwa na umoja wa kusaidiana katika kupata uongozi.

Kama alivyosema Rais Samia, anataka lililoanzishwa na wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), pia liendelezwe na wanawake wa vyama vingine vya siasa.

Wanawake wana nguvu kubwa na pia ndiyo wanaoongoza kwa idadi ya watu kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.


Wao ndiyo wapigakura wakubwa wakiamua jambo lao hakuna wa kuwazuia. Wakijipanga vizuri na wakilitaka jambo ni rahisi kulipata. Cha muhimu ni kuepuka mgawanyiko na kurubuniwa kwa kupandikizwa chuki za kuchukiana wenyewe kwa wenyewe na kuchafuana kwenye majukwaa.

Wanawake wanaweza kuleta mabadiliko makubwa na yameanza kuonekana kupitia kwa Rais Samia.

Kwenye familia nyingi viongozi wanaosimamia au kuendesha familia zao ni wanawake, hata sasa kwenye shughuli mbalimbali kama mwanamke asipokuwa msimamizi mambo hayaendi sawa.

Hii inadhihirisha kuwa wanawake ni jeshi kubwa na wanapojiamini na kudhamiria kufanya jambo lako, hakuna anayeweza kulizuia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hongera Rais kuondoa nyungu kuleta chanjo

**WAKATI** ugonjwa wa UVIKO-19 unaingia nchini, kulikuwa na sintofahamu, kutokana na baadhi ya watu kuamini kuwa njia ya kuudhibiti ni kujifukiza au 'kupiga nyungu', badala ya kutumia dawa zinazoelekezwa na wataalamu wa afya.

Katika mazingira hayo, umma uligawanyika wakiwapo wanaoamini kujifukiza na wale wanaozikubali dawa za hospitali na hivyo kuwapo kwa makundi mawili yenye mtazamo tofauti kuhusu ugonjwa huo.

Hata hivyo, Rais Samia Suluhu Hassan, anapoingia madarakani, anaanzisha kampeni ya kutoa elimu na kuhamasisha jamii kupata chanjo ya ugonjwa huo, huku akiwa mtu wa kwanza kuchanjwa.

Uamuzi wake wa kujitokeza hadharani kuchanja ulibadilisha upepo na hivyo kuwafanya Watanzania kujitokeza kwa katika vituo mbalimbali vya kutolea chanjo, kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya UVIKO-19.

Yeye hakupinga suala la kupiga nyungu, lakini msisitizo wake ulikuwa ni jamii kutambua umuhimu wa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya badala ya kujifukiza majani bila kujua madhara yake ya baadaye.

Hivyo, Rais anapoanza mwaka mwingine wa uongozi wake, ni wazi amesaidia kuelimisha Watanzania kutoka kwenye upigaji wa nyungu hadi kupata chanjo ya UVIKO-19 ambayo awali waliiona kama adui mkubwa.

Kufikia Desemba mwaka jana, serikali ilipanga kufikia asilimia 70 ya watu waliochanja ikiwa ni sehemu ya mkakati wa dunia wa kupambana na ugonjwa huo wa UVIKO-19.

Hatua ya kuhamasisha chanjo, ilitokana na kuthibitishwa kisayansi kwamba, ili kupata kinga kamili dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19, angalau asilimia 70 ya watu wote wawe wamepata chanjo hiyo nchini.

Ingawa kama ilivyo katika maeneo mengine duniani, mwanzo wa mchakato wa chanjo hiyo, ulikuwa na taarifa nyingi za upotoshaji, baadhi ya watu wakisema kuwa chanjo si za kawaida, hivyo wana mashaka na ufanisi wake.

Hoja nyengine potofu iliosikika nchini na kwingineko ni kuwa chanjo hizo zina madhara makubwa kwa watumiaji wake, ikiwamo kusababisha vifo, kuvuruga hedhi, kuharibu nguvu za uzazi kwa wanaume na wanawake na kushambulia mfumo wa vinasaba na kuwafanya watu kuwa 'mazombi'.

Lakini hoja hizo kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) hazikuwa na mashiko na ndilo lenye dhamana ya kusimamia masuala yote ya kiafya duniani ikiwamo kupasisha ufanisi wa dawa na chanjo.

Wataalamu wa WHO wanabainisha kuwa chanjo zote zilizopitishwa za ugonjwa zilikuwa ni salama kwa matumizi ya binadamu na zimefanyiwa utafiti na uchunguzi wa kutosha wa kisayansi na kiutabibu.

`Sasa tuko mwaka mwingine wa 2023, ni vyema kampeni za kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kupata chanjo zikaendelea ili kuhakikisha kila anayetakiwa kuchanja, basi apate huduma hiyo.

Ninaamini kwamba, pamoja na jitihada za serikali kwa kupindi cha miaka miwili iliyopita, wapo baadhi ya watu ambao huenda kwa kutoelewa, au kwa kuamini nyungu, bado hawajajitokeza kuchanja.

Hivyo, suala la kuendelea na kasi ya kutoa elimu na uhamasishaji kwa wananchi ili wakubali kupata chanjo hiyo, ni la muhimu wakati huu ambao Rais Samia anaanza mwaka wa tatu akiwa madarakani.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, ugonjwa huo bado upo, hivyo, si vyema watu kubweteka na kudhani wako salama, badala kila mmoja achukue hatua zitakazomfanya awe salama dhidi ya UVIKO-19.

Tayari Rais ametuonyesha njia salama dhidi ya ugonjwa huo ni kupata chanjo inayoelekezwa na wataalamu wa afya na si vinginevyo kama ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakidhani.

Chanjo kwa mujibu wa serikali, ni hiari, lakini jamii isibweteke kwa huo uhiari, bali jambo la msingi ni usalama wa afya dhidi ya ugonjwa huo, ambao ukweli ni kwamba unategemea chanjo ya kuudhibiti.

# Waziri aomba uharaka usikilizwaji hoja 3 SADC

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, amewasilisha hoja tatu kwenye mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), akitaka kuongezwa kasi katika utekelezaji.

Mkutano huo uliofanyika hivi karibuni nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa siku mbili, ulioanza Machi 18 na kuhudhuriwa na wawakilishi kutoka Tanzania akiwamo Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde.

Hoja alizoziwasilisha ni pamoja na hatua iliyofikiwa kuhusu tafsiri ya nyaraka muhimu za SADC katika lugha ya Kiswahili, ujenzi wa sanamu ya Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Nyerere na Mpango wa Kanda wa ununuzi wa pamoja wa vifaa vya afya unaoratibiwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

"Utekelezaji wa tafsiri ya nyaraka muhimu za SADC katika lugha ya Kiswahili upo katika hatua za kumpata mzabuni wa kufanya kazi hiyo na ujenzi wa sanamu ya Baba wa Taifa unaendelea, kazi hiyo inatakiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2023.

"Kuhusu Mpango wa Kanda wa ununuzi wa pamoja wa vifaa vya afya MSD inaendelea na jukumu hilo hivyo ninawaomba nchi wanachama kuongeza kasi ya kuitumia bohari hiyo kwa kuwa manufaa yake ni makubwa hususani kwenye kupunguza gharama za ununuzi wa dawa na vifaa tiba," alifafanua.

Waziri Mkuu wa DRC, Jean-Michel Nyenge, Waziri wa Mtangamano wa Kikanda wa DRC, Didier Mukanzu na Katibu Mtendaji wa SADC, Elias Magosi, walitaja maeneo muhimu ya kuwekewa mkazo ili kupanua wigo wa mtangamano na kuongeza kasi ya maendeleo baina ya nchi wanachama.

Walitaja maeneo hayo kuwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu, ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani ya bidhaa za madini, ngozi na kilimo, kuwa na nishati ya umeme ya uhakika, usawa wa kijinsia katika siasa na zaidi ya yote ni umuhimu wa kuimarisha amani na usalama katika kanda.

Pia walisema maeneo hayo yameainishwa vyema katika Mpango Mkakati wa Maendeleo wa Kanda (2020-2030) na Sekretarieti ya SADC, imeahidi kuendelea kuratibu na kuhamasisha utekelezaji wake.

Miradi 11 ya Tanzania imeingia katika mpango huo ikiwamo uendelezaji wa sekta ya maji katika mto Songwe, usindikaji wa ngozi, uzalishaji wa mbolea, uchumi wa buluu, nishati, utafiti, elimu na utengenezaji wa dawa za binadamu na wanyama.

# Bunge laridhishwa kasi ujenzi mradi Kinyerezi I

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeipongeza serikali kwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya kuzalisha umeme wa Kinyerezi I, unaotekelezwa na Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO), utakaoondoa tatizo la umeme na kukuza uchumi wa nchi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dunstan Kitandula, aliyasema hayo juzi baada ya kutembelea kituo cha kuzalisha umeme wa kutumia gesi asilia cha Kinyerezi I kitakachozalisha megawati 185.

"Kama Kamati tumeona mradi unaendelea vizuri na mitambo mitatu tayari imeanza kuzalisha megawati 135, bado mtambo mmoja ambao utekelezaji wake unaendelea vizuri," alisema Kitandula.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Jumla ya pesa zitakazotumika hadi mradi huu ukamilike ni Dola za Marekani milioni 188 na hizi ni jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kwa ufadhili huu tuna uhakika utaongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika na wenye ubora na kuwezesha maendeleo mbalimbali kwenye viwanda vikubwa na vidogo na maendeleo ya kijamii," alisema Byabato.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, alisema mradi huo ulianza mwaka jana na kazi iliyofanyika mitambo mitatu kati ya minne imeingiza umeme kwenye Gridi ya Taifa.

"Ifikapo mwishoni mwa Aprili 2023 mtambo wa nne utakuwa tayari kuanza kuzalisha umeme. Hivyo natumia fursa hii kuwashukuru wateja kwa uvumilivu wakati huu mradi unaendelea kujengwa na nawapongeza wafanyakazi kwa kazi ngumu yenye kuleta mafanikio kwa taifa letu," alisisitiza.

Wajumbe wa kamati hiyo, Consatine Kanyasu na Jesca Kishoa, waliipongeza TANESCO kwa kutekeleza miradi ya maendeleo na kuomba kuwapo ufuatiliaji wa karibu ili ukamilike kwa wakati na kufikia malengo yalitakiwa.




Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Tabia Maulid Mwita (katikati waliosimama), akishuhudia utiaji saini wa mkataba wa ushirikiano wa kibiashara kwa ajili ya utengenezaji wa jezi na vifaa vya Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), kati ya Benki ya CRDB iliyowakilishwa na Ofisa Mkuu wa Biashara, Boma Raballa (kulia), Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF) lililowakilishwa na Rais wake, Abdullatif Ali Yassin (katikati) pamoja Kampuni ya Ubunifu wa Mavazi ya Sheria Ngowi chini ya Sheria Ngowi mwenyewe (kushoto), mwishoni mwa wiki Zanzibar. Wengine; Makamu wa Rais wa ZFF, Hafidh Mohamed Ali (wa pili kushoto waliosimama), Katibu wa ZFF, Hussein Ahmada Vuai na wanasheria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DAWASA yawakumbuka wakazi wa Mivumoni

**Na Joseph Mwendapole**

WAKAZI wa Mivumoni jijini Dar es Salaam wameanza kunufaika na huduma ya majisafi baada ya kukamilika kwa mradi mkubwa wenye thamani ya Sh. bilioni 65.

Mradi huo unatekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira DAWASA na ulifadhiliwa na Benki ya Dunia (WB).

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Huduma kwa Wateja wa DAWASA, Linah Kikoti, wakati akizungumza na wananchi waliofika kwenye madawati ya huduma kwa wateja.

"Hatua hii imekuja baada ya kukamilika kwa mradi wa usambazaji maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo uliotekelezwa na DAWASA kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ukihusisha ujenzi wa matangi matatu ya kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita milioni tano kila moja katika maeneo ya Vikawe, Mbweni, na Tegeta 'A'," alisema.

Alisema wakazi wa mitaa ya Tegeta 'A', Goba Mpakani na Nyakasangwe wamejitokeza kwa wingi katika madawati ya huduma kwa wateja yaliyofunguliwa katika mitaa hiyo ili DAWASA kuwasogezea huduma zaidi wananchi majisafi.

Alisema mamlaka imefungua madawati maalumu ili kuwafikia wananchi wengi kwa haraka katika maeneo yao na kusaidia huduma kuwafikia kwa wepesi zaidi.

Aliwasisitiza wananchi kutumia fursa hiyo kufika kwa wingi ili waweze kuunganishwa na huduma ya majisafi.

"Hii ni nafasi muhimu ya mwananchi kupata huduma ya maji kwa urahisi kabisa, niwaombe wajitokeze kwa wingi ili isitokee mwananchi akakosa huduma ya majisafi," alisema.

Akizungumzia huduma hiyo, Mjumbe wa Shina namba 10 Goba Mpakani, John Jelle, aliishukuru DAWASA kwa kufika katika mitaa yao kwa kuwa kufanya hivyo wanapata fursa yakuwafikia wateja wengi zaidi.

"Huduma ya maji imetufikia, tunaishukuru sana serikali ya awamu ya sita, zoezi linaloendelea katika mitaa yetu ni kuwaunga wateja na majisafi, kwa DAWASA kuwa hapa tunategemea kila mwananchi atapatiwa huduma ya majisafi," alisema mjumbe huyo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Aweso aagiza wanaoomba maji kuunganishiwa ndani ya siku 7

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewataka watumishi wa wizara hiyo kuacha urasimu wa kuwaunganishia maji wananchi na kuagiza ndani ya siku saba mteja aliyeomba kupata huduma hiyo awe ameipata.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya mafanikio ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan, madarakani kwenye sekta ya maji, yaliyoandaliwa na Kituo cha Clouds Media.

"Mkataba unasema mwananchi akitaka kuunganishiwa maji basi ndani ya siku saba anatakiwa awe ameunganishiwa, sio anakuja mtu anazungushwa mara mita hakuna, mwingine anatoa kitu kidogo anapata huduma. Kwani kwake mita imetoka wapi? Tuache hiyo tabia," alisema Aweso.

Alisema katika miaka miwili ya Rais Samia madarakani mafanikio mengi yamepatikana katika sekta ya maji ikiwamo ujenzi wa miradi zaidi ya 157.

Alisema Rais Samia alipatia Wizara ya Maji fedha za ugonjwa wa UVIKO Sh. bilioni 135 ambazo zimefanikisha kutekeleza miradi 218, vijijini miradi 174, mijini 44.

Mbali na mafanikio hayo, Awesso alisema kila mwaka mvua zimekuwa zikinyesha, lakini maji yanapotea bila kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye.

Alibainisha kuwa uzoefu walioupata kupitia mabadiliko ya tabianchi mwaka jana imewapa funzo na kuwataka wananchi kulinda na kutunza rasilimali za maji.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Cyprian Luhemeja, aliwatahadharisha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) endapo hawatakuwa makini ifikapo mwaka 2025 kiwango cha maji kitapungua hadi asilimia 80.

Luhemeja ambaye alikuwa Mtendaji Mkuu wa DAWASA kabla ya kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, alisema Dar es Salaam ni jiji kubwa la kibiashara linalochangia asilimia 75 ya mapato na kwa sasa huduma hiyo inapatikana kwa asilimia 95.

"DAWASA kuweni makini mwaka 2023 maji yanapatikana kwa asilimia 95, ukipiga hesabu mwaka 2025 kama hamna kazi mnayofanya tutakuwa asilimia 80," alisema Luhemeja.

Alibainisha kuwa jiji hilo linakuwa kwa kasi ni lazima wawe na kasi itakayoendana na kukua kwa mji endapo watataka kuwa na viwango sawa.

"Kazi kubwa inafanyika yamebaki maeneo machache ikiwamo Mwanagati, Kitunda, Kivule na Chamanzi, tayari Sh. bilioni 40 zimetengwa kwa ajili ya kufanya usambazaji kwenye maeneo hayo," alisema.

Akizungumzia miradi ya maji iliyokamilika vijijini, Luhemeja alisema miradi 382 imekamilika na zaidi ya watu milioni mbili wanapata huduma hiyo, huku vituo 3,400 vikijengwa kwenye vijiji 684.




Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Apps ya Wasichana, Carolyne Ekyarisiima (katikati) akiwa na wawakilishi wa Tigo na waratibu wa Tuzo za WSIS 2023 baada ya kuibuka washindi kati ya mabingwa watano waliochaguliwa katika tuzo hizo kwenye kipengele cha E-employment iliyohusisha miradi 190 iliyoteuliwa ulimwenguni, tuzo hizo zilifanyika Geneva, Uswizi Machi 14. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TRC yatakiwa kuleta matokeo chanya

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), Jeryy Silaa, ameitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi) kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuhakikisha uwekezaji unaofaywa kupitia maboresho ya njia ya Reli ya Kati, Chuo cha Reli na Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR unakuwa na matokeo chanya kwa taifa.

Akizungumza alipotembelea stesheni, karakana na Chuo cha Reli mkoani Tabora, Silaa alisema Shirika la Reli ni miongoni mwa mashirika ambayo serikali imewekeza zaidi ya Sh. trilioni 15 lengo likiwa kuliwezesha kujitegemea baada ya uwekezaji huo kukamilika.

"Kwa uwekezaji uliowekwa katika Sekta ya Usafiri kupitia TRC tunapaswa kujipanga sawa sawa sababu wananchi hawatawaelewa kama uwekezaji huu utakamilika na tija isionekane," alisisitiza.

Aliitaka wizara kupitia TRC kuongeza nguvu kwenye usimamizi wa reli ya kati kwa kuwa imeonekana nguvu kubwa imewekezwa kwenye reli ya kisasa na kupunguza ufanisi kwa reli hiyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya TRC, Profesa John Kondoro, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwekeza fedha kwa TRC kwa kuwa kukamilika kwa miradi yote ya uboreshaji, ununuzi na ujenzi utarahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo na hivyo kupunguza gharama za bidhaa.

Mwenyekiti Prof. Kondoro aliihakikishia Kamati ya Bunge kuwa TRC imejipanga kwa uendeshaji wa reli ya kisasa kwa kuweka mpango madhubuti wa biashara wa muda mfupi na muda mrefu ili kujipima kwa vigezo maalum kulingana na fedha iliyowekezwa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Amina Lumuli, alisema mpango unaotekelezwa wa maboresho ya miundombinu ya reli umehusisha ujenzi wa chuo kikubwa kitakachofundisha kozi mbalimbali za usimamizi na uendeshaji wa reli zote mbili lengo likiwa kuongeza wataalamu.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), iko katika ziara mkoani Tabora na imekagua miundombinu ya reli na Chuo cha Reli ili kuona utayari wa shirika hilo katika uandaaji wa wataalamu na uendeshaji wa reli ya SGR baada ya miradi hiyo kukamilika.

# Polisi yanasa bastola ya wahalifu, risasi 71

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha limekamata bastola moja, aina ya CZ 75 LUGER yenye namba za usajili A487385 pamoja na risasi 71 za silaha hiyo iliyokuwa inatumiwa na wahalifu.

Aidha, kwa nyakati tofauti wamefanikiwa kukamata watuhumiwa 11 wakiwa na mirungi bunda 528 yenye uzito wa zaidi ya kilogramu 162, ambayo walikuwa wakiisafirisha kwa kutumia magari na pikipiki.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, risasi hizo, zilikutwa kwenye nyumba Kijiji cha Ilkyurei, Kata ya Kiranyi, Wilaya ya Arumeru, wakati wa mwendelezo wa operesheni maalum ya kuwasaka wahalifu inayoendelea. "Katika operesheni hii maalum ya kuwasaka wahalifu, tulifanikiwa kukamata bastola moja na risasi saba, lakini kwa bahati mbaya watuhumiwa waliokuwa wanatumia silaha hiyo walifanikiwa kukimbia baada ya Polisi kuikaribia nyumba hiyo na msako mkali unaendelea dhidi yao," alisema.

Kuhusu watuhumiwa 11 waliokamatwa wakisafirisha dawa hizo, Masejo alisema kuwa upelelezi unaendelea ukikamilika, jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria kujibu tuhuma zinazowakabili.

Katika hatua nyingine Kamanda Masejo alisema ofisi yake kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, wamefanikiwa kumfikisha mahakamani mtu mmoja Julius Mollel (27), mkazi wa Kijiji cha Lashaine Wilaya ya Monduli, kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi wa darasa la pili mwenye umri wa miaka minane na kuhukumiwa kifungo cha maisha jela.

Kamanda Masejo alisema wanaendelea kukutana na wananchi pamoja na viongozi wa kata, mitaa na vijiji, kutoa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia na masuala ya usalama, ikiwamo umuhimu wa kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi, katika maeneo yao ili kukomesha matukio ya uhalifu.

"Pamoja na kutoa elimu kwa jamii pia niiombe sana jamii kuacha tabia ya kujihusisha na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake, lakini ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi dhidi ya watu wanaohusika na vitendo vya aina hiyo na atakayebainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yao," alisema.

Aliwaomba wananchi kutoa taarifa polisi dhidi ya wahalifu katika maeneo yao kwa sababu wanaishi ndani ya jamii.



## Serikali kuleta mizani ya kidijitali kuondoa udanganyifu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

BODI ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani (WRRB) imesema serikali inafikiria kuleta nchini mizani ya kidijitali ili kuondoa udanganyifu katika uuzaji wa mazao kwa wakulima.

Meneja Mipango na Uhamasishaji wa Bodi hiyo nchini, Sura Ngatuni, alisema serikali inaamini mizani ya kidijitali itakapoanza kutumika itasaidia wakulima na ghala kuu kukabiliana na wizi unaofanywa na wajanja.

Ngatuni alikuwa akizungumza jana Wilaya ya Babati, mkoani Manyara na wadau wa kilimo katika mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani.

"Hivi sasa tunaendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau wa kilimo kuhusu matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani, ambapo mafunzo haya yanatolewa kwenye mikoa mitatu ya Manyara, Njombe na Rukwa.

"Pia mfumo huu utaondoa kuchanganya uchafu na mazao ili kuongeza uzito, anapouza mkulima, kwa kuwa mazao yatakapokuwa yanapimwa ghala kuu, watakuwa wanaona,"alisema Ngatuni.

Kuhusu anguko la bei ya mazao, Ngatuni, alisema hamna fungu lolote linalotolewa na serikali kufidia wakulima bei ya mazao inaposhuka.

Aidha, alisema linapotokea anguko la soko duniani na linakuja kuligusa taifa letu, hakuna sababu ya mkulima kuilaumu serikali.

Naye Ofisa Mwandamizi Uendeshaji Biashara kutoka Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Justa Martine, alisema kwa sasa TMX inafanya mauzo ya papo kwa papo.

Akifungua mafunzo hayo juu ya mfumo huo, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, alisema panapotokea vikwazo au ukinzani juu ya mfumo, hujitokeza matatizo ya uelewa mdogo juu ya mfumo.

**"Hivi sasa tunaendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau wa kilimo kuhusu matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani, ambapo mafunzo haya yanatolewa kwenye mikoa mitatu ya Manyara, Njombe na Rukwa.**

# Mapitio kesi ya kupinga vijiji kuwa pori tengefu kusikilizwa

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, Mei 4 mwaka huu itaanza kusikiliza ombi la mapitio ya shería kuhusu kesi ya kupinga amri ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kutangaza ardhi ya vijiji vya Loliondo, vilivyoko Wilaya ya Ngorongoro kuwa Pori Tengefu la Pololeti.

Kesi hiyo namba 21 ya mwaka jana inasikilizwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Joachim Tiganga.

Sababu za kesi hiyo kusogezwa mbele ni pamoja na serikali kuomba muda wa kuwasilisha mapitio ya mwanasheria wa serikali kuhusu katazo hilo.

Jaji Tiganga amesogeza mbele tarehe ya mapitio ya shauri hilo linalohusu tangazo la Waziri wa Maliasili na Utalii, (G.N Namba 421 ya Juni 17, 2022) ili kumpa nafasi Wakili wa Serikali, Mkama Msalama, kuwasilisha hati ya kiapo kinzani mahakamani humo.

Kabla ya kuahirisha shauri hilo, Jaji Tiganga, alitoa muda wa siku saba kwa Wakili wa Serikali Mkama Msalama, kuhakikisha anapeleka mahakamani hapo kiapo kinzani cha maombi hayo.

Katika shauri hilo waliowasilisha ombi hilo ni wananchi watano kutoka vijiji vilivyoathiriwa na tangazo hilo.

Wananchi hao wanaiomba mahakama iagize serikali kuondoa zuio lililoko la kutoingia kwenye eneo lenye ukumbwa wa kilomita za mraba 1,502, ambalo wamekuwa wakilitumia kwa ajii ya malisho ya mifugo yao na shughuli za kiimani.

Aidha, wanaiomba Mahakama kutengua tangazo la serikali kupitia G.N 421 la Juni 17, 2022, kwamba ni batili na limetangazwa kinyume na sheria.

Katika ombi lao wananchi hao wanadai kuwa katika uamuzi huo wa serikali, hawakushirikishwa wananchi kama sheria inavyotaka.

Pia wanaiomba Mahakama itamke na kuizuia serikali na mawakala wake wasifanye operesheni yeyote kwenye eneo hilo.

Upande wa utetezi katika kesi hiyo, unawasilishwa na mawakili Joseph Shangay, Denis Moses na Hamis Mayombo.



Mbunge wa Viti Maalum Vijana Manyara, Asia Halamga (kushoto), akizungumza mbele ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu kurasimishwa makazi kwa watu 978 wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Hospitali ya Bombo kuanza kupima usikivu kwa watoto

**Na Oscar Assenga,** TANGA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo, inatarajia kuanza kutoa huduma ya upimaji usikivu kwa watoto wachanga baada ya kuzaliwa.

Matumaini kuhusu ujio wa huduma hiyo, yalitangazwa jana jijini humo na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Masikio, Pua na Koo, Mohamed Sachedin, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Afya ya Kinywa na Meno Duniani.


"Kuanzishwa kwa huduma hii kutaifanya hospitali yetu kuwa miongoni mwa hospitali chache zinazotoa huduma ya kupima watoto wachanga.

"Kwa mwaka huu, tayari tumewaona wagonjwa 1,000 kwenye kliniki ya pua, masikio na koo. Kati ya hao, asilimia 50 walikuwa na shida ya masikio na usikivu."

Kwa mujibu wa Dk. Sachedin, shida ya usikivu huanza wakati mtoto anapozaliwa na kuendelea mpaka anapofikia uzeeni, hivyo ni vyema watoto kupimwa usikivu wanapozaliwa.

Alifafanua kuwa ni vyema kujali afya ya sikio lako na kila linapopata shida ni muhimu kufika kwenye kituo cha afya, huku akitoa wito kwa watu wanaofanya kazi sehemu zenye kelele, kutumia vizuizi ili kuepusha madhara ya sauti kubwa ambayo baadaye husababisha shida ya usikivu.

Maadhimisho ya afya ya kinywa na meno kitaifa kwa mwaka huu yanafanyika mkoani Kigoma.





# Serikali yatenga bil.44/- ujenzi Chuo cha Reli

**Na Halima Ikunji,** TABORA

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh.bilioni 44 kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa Chuo cha Reli kitakachokuwa na viwango vya kimataifa.

Chou hicho kitatoa mafunzo ya teknolojia mpya ya reli nchini kupitia ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Tabora-Isaka.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Nchini (TRC), Amina Lumuli, wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi wa SGR kipande cha Tabora-Isaka kwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) wakati wa ukaguzi wa karakana ya miundombinu ya mradi huo.

Lumuli alisema kupitia chuo hicho Watanzania watapata nafasi ya kujifunza teknolojia mpya ya reli ya kisasa.

Alieleza kuwa chuo hicho kinatarajiwa kujengwa eneo la Marabi, Kata ya Cheyo Manispaa ya Tabora, kitakuwa na ukubwa wa ekari 183.1.

Alisema mkandarasi wa ujenzi wa chuo hicho ameshakamilisha michoro na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Lumuli alisema chuo hicho kitawezesha kutoa mafunzo katika teknolojia mpya ya reli ambayo itakuwa na vitendea kazi na miundombinu ya kisasa.

Sambamba na hilo kutakuwa na ukarabati mwingine utafanyika katika Kampasi ya Morogoro ambayo imetengewa Sh.milioni 450 kupitia mradi wa SGR kwa kipande cha Dar-es-Salaam-Tabora ambayo itahusisha majengo, miundombinu ya majisafi na taka pamoja na mifumo ya umeme na mawasiliano.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Jerry Silaa, alisema mpaka sasa kazi kubwa inayofanyika imeanza kuonekana katika Mkoa wa Tabora kupitia fedha zinazotengwa na kutolewa na serikali.

Silaa alisema serikali imetenga kiasi hicho kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho na ukarabati wa Kampasi ya Morogoro kutengewa Sh.milioni 450 ikiwa na chuo kufanya uwekezaji kwa muda wa miaka mitatu kwa kiasi cha Sh.bilioni 914.2.




Mkuu wa Kitengo cha Polisi wa Usalama Barabarani Wilaya ya Tarime, ASP Barnabas Irumba, akiongea kwenye hafla ya kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani iliyofanyika kiwilaya katika mji wa Nyamongo ikidhaminiwa na mgodi wa Barrick North Mara. Mgodi huo, uliwapatia waendesha pikipiki kofia ngumu na jaketi maalum za usalama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watatu mbaroni tuhuma wizi wa mafuta mradi wa SGR

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linawashilikia watu watatu kwa tuhuma za wizi wa mafuta aina ya dizeli lita 302 yanayotumika katika shughuli ya ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR).

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Leonard Nyandahu, alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari.

Alisema waliwakamata watuhumiwa hao wakiwa na vifaa mbalimbali ikiwamo pikipiki zilizotelekezwa pamoja na dawa za kulevya baada ya kufanyika kwa msako kuanzia Februari 28 hadi Machi 20, mwaka huu.

"Tumekamata dawa za kulevya aina ya bangi kilo 22, saruji mifuko mitatu, magodoro mawili, pikipiki nne zilizotumika kwenye uhalifu, printa moja, kompyuta moja, runinga mbili, mbolea kilo 30 na betri 10 za magari," alisema Nyandahu.

Aidha, alisema pia Jeshi la Polisi limeokota pikipiki tatu ambazo zilitelekezwa maeneo tofauti, huku akibainisha kuwa wamekamata watuhumiwa 10 ambao walihusika katika matukio ya wizi.

Kamanda Nyandahu aliwasihi wananchi kuendelea kutoa taarifa za uhalifu pamoja na kuacha kuhujumu mradi wa SGR kwa kuiba vifaa vya ujenzi na mafuta, huku watuhumiwa wote waliokamatwa wakitarajiwa kufikishwa mahakamani hivi karibuni.

**"Tumekamata dawa za kulevya aina ya bangi kilo 22, saruji mifuko mitatu, magodoro mawili, pikipiki nne zilizotumika kwenye uhalifu, printa moja, kompyuta moja, runinga mbili, mbolea kilo 30 na betri 10 za magari," alisema Nyandahu.**

# Mradi wa majisafi kunufaisha wakazi vijiji vitano Shinyanga

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa vijiji vitano vya Kata ya Kagongwa na Isaka wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wanatarajia kunufaika na mradi wa majisafi na salama wa Isaka-Kagongwa kutoka Ziwa Victoria.

Mradi huo utawawezesha wakazi hao kuondokana na matumizi ya maji machafu ya kwenye madimbwi na visima vifupi pamoja na wanyama wanaowafuga.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Julieth Payovela, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa kwa Kamati ya Bunge ya Maji na Mazingira.

Alisema mradi huo utahudumia vijiji vya Mwalugulu, Kilimbu, Butondolo pamoja na Kijiji cha Itogwanholo kwa Sh. bilioni 4.256.

Mhandisi Payovela alisema utekelezaji wa mradi huo ulianza Machi 16, mwaka jana, mpaka sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 50 na unatarajia kuhudumia wananchi ifikapo Juni 30, mwaka huu.

Alisema mradi huo unatekelezwa na mkandarasi wa Kampuni ya PNR Services Ltd ya jijini Dar-es-Salaam.

Mhandisi Payovela alisema awamu ya kwanza ya mradi utahudumia vijiji vya Jana, Butondolo na Itogwanholo vilivyopo katika Kata ya Jana na Isaka.

Alisema awamu ya pili itahusisha vijiji vya Mwalugulu na Kilimbu vilivyoko Kata ya Mwalugulu na kuwataka wananchi kuutunza mradi huo ili uendelee kuwanufaisha.

"Mpaka sasa tumeshamlipa mkandarasi Sh. bilioni 1.4 sawa na asilimia 33 ya mkataba, kati ya hizo Sh. milioni 961.9 ni malipo ya hati namba moja, mbili na tatu na Sh. milioni 446.1 ni malipo ya awali, hivyo mradi utakamilika kwa wakati,"alisema Mhandisi Payovela.

Hata hivyo alisema wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa bomba za chuma na kiwanda cha uzalishaji wa aina hizo kipo kimoja nchini hali inayosababisha mahitaji kuwa makubwa kuliko uwezo wa kiwanda.

Diwani wa Kata ya Isaka, Pazi Majuto, alisema wananchi wa vijiji hivyo wanatumia maji ya madimbwi pamoja na mifugo hali inayosababisha kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko.

Alisema mradi huo utakapokamilika utaondoa tatizo hilo kwa wananchi na watautunza ili uendelee kunufaisha vizazi vijavyo kama ambavyo sasa wanatunza vifaa vya ujenzi wa SGR.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alisema maeneo yote ya pembezoni watahakikisha yanapata majisafi na salama kwa kuchimba visima virefu na vifupi au kupelekewa maji ya Ziwa Viktoria.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maji na Mazingira, Jackison Kiswaga, aliwataka wamiliki wa viwanda vya uzalishaji wa bomba za chumba na plastiki kuongeza kasi ya uzalishaji ili miradi ya maji ikamilike kwa wakati.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 21, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12
Ni mbinu mpya kuelimisha watoto tabianchi kufunzwa kwa sanaa, uchoraji

Ukurasa 13
Njia tofauti kuunda maneno ya Kiswahili Kenya ikirahisisha, Tanzania ugumu



Ukurasa 14
**Kasi ndoa za jinsia moja ni kuiandaa dunia kuwa 'jangwa'**

TEKNOLOJIA

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

MIAKA 2 YA MAMA

# Tanzania inapong'ara kilimo, chakula Afrika

•Wasomi, wataalamu SIDO, SUA, NYUMBU wawe namba 1

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametangaza maono makubwa ya taifa na fursa ya uhakika ya kuilisha Afrika chakula kwa kutumia wakulima na ardhi ya Tanzania.

Anayafanya hayo kupitia mkakati wenye mipango kadhaa ikiwamo kuboresha kilimo, kuwajengea vijana uwezo yote hayo yakipewa nguvu na mfuko wa kitaifa wa kuimarisha kilimo (AGTF) utakaoanzishwa wakati wowote kuanzia sasa.

Ni mambo anayoyatangaza hivi karibuni wakati akizindua jukwaa la mifumo ya chakula barani Afrika, jijini Afrika Dar es Salaam.

Anawahakikishia Watanzania kuwa katika mkakati huo serikali inatoa pembejeo bora kuanzia mbegu, zana, mbolea na viuadudu kwa wakulima na mafunzo ya kilimo yanayolenga kuwaandaa na kuwapika vijana wakulima stadi na waelewa wa jukumu hilo.

Rais anasema kwa kuanza vijana 800 wameandaliwa na watapata mafunzo na kunufaika na maeneo ya uzalishaji yaliyoandaliwa kwa maana ya mashamba na kwamba Tanzania ina nia ya dhati ya kutumia mamilioni ya hekari za ardhi bora ya kilimo ikiwamo ile ya umwagiliaji pia.

Anabainisha kuwa zipo hekta milioni 44 za ardhi bora kwa kilimo na nyingine milioni 29 mahsusi kwa kilimo cha umwagiliaji.



Trekta ya kulimia, kuvunia na kubangua mazao inayoundwa na Taasisi ya CAMARTEC ni teknolojia muhimu kwenye uwekezaji wa kimkakati wa kilimo unaoanza sasa. **PICHA: MTANDAO**

**SI LAKUACHWA**

Pamoja na nia nzuri ya uzalishaji na kuinua sekta ya kilimo ili kuwa na nafsi ya kuilisha Afrika na dunia, suala la kuendeleza na kutumia teknolojia ya ndani kwenye mradi huo lina umuhimu wa kipekee na ikiwezekana serikali ilitazame.

Pamoja na kuhitaji zana kama matrekta mfano ya kampuni za kigeni ili kulima ardhi kipaumbele pia kitolewe kwa wataalamu na wabunifu wa ndani na viwanda vya Tanzania ili vizalishe baadhi ya vifaa, zana na bidhaa vikiwamo viautilifu vya asili vitakavyotumika kwenye mkakati huo.

Mradi huo ufanikishe pia kutumia zaidi kampuni, taasisi na viwanda vya Tanzania kama SIDO, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), Shirika la Jeshi la Wananchi la NYUMBU na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO) vilivyoko Arusha kuwekeza teknolojia ya ndani kufanikisha safari ya mapinduzi ya kilimo.

Uwekezaji mkubwa wa mashine za kusukuma maji, jenereta, pampu, nyingine za kuvuna, kukoboa, kusindika na kudhibiti upotevu wa mazao mashambani utumie teknolojia na wahandisi wa ndani kufikia azma hiyo.

Wanapoalikwa wawekezaji kwenye mradi huo kwa mfano watengeneza zana kama wauzaji na waingizaji wa matrekta mfano John Deere na Massey Ferguson Limited yote ya Marekani, Ford au Power Tiller ya China, serikali isiwasahau kuwapa nafasi wataalamu wa ndani kama TEMDO kutengeneza majembe 'disc', 'haro' vifungashio vya mbegu na mbolea ili pia teknolojia na uhandisi wa ndani uwe na nafasi.

Aidha, ikiwezekana kampuni kama General Tyre, iingie kwenye mradi kwa kupewa nafasi ya kuzalisha matairi, mipira ya matrekta hayo badala ya kila kitu kutoka nje.

Ni vyema vitu kama hivyo viandaliwe hapa nchini ili kuinua teknolojia, wabunifu na wahandisi wa Tanzania ili hatua kwa hatua wainuke na miaka ijayo ikiwezekana kuondoa kuingiza matrekta hayo kutoka nje na badala yake yazalishwe nchini.

Pamoja na hayo kilimo na uwekezaji unaokuja utumie wataalamu wa uhandisi wa kilimo kutoka NYUMBU, TEMDO, SIDO, CAMARTEC, kuzalisha kuunda vifaa kama pumpa za kilimo zinazoendeshwa kwa umeme jua (sola), gesi hata upepo ujuzi utumike ule unaotoka Tanzania siyo kuagiza kila kitu kutoka nje jambo ambalo pia litisaidia kuinua na kufanikisha upatikanaji ajira, maendeleo ya sayansi na utafiti.

Ikiipendeza serikali ni vyema uwekezaji huo mkubwa wa kilimo uangalie namna ya kuwatumia wataalamu wa kutengeneza zana za kilimo mfano Shirika la Mzinga, wahandisi wa kiwanda cha UFI, SIDO na hata wale wa kilichokuwa kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya -ZZK kutengeneza baadhi ya mashine mfano maksai (plau) kwa kuyeyusha vyuma badala ya kuagiza vitu hivyo nje.

Ni wazi kuwa Tanzania ina wataalamu wa kufanikisha kilimo mfano walioko TEMDO, SIDO, CAMARTEC, wengine waliofanyakazi UFI, ZZK ambao wana teknolojia ya kuyeyusha vyuma na

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA JENIFER GILLA

# Ni mbinu mpya kuelimisha watoto tabianchi kufunzwa kwa sanaa, uchoraji

TANZANIA na mataifa yote duniani yanapambana kuzuia madhara ya athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo yameshaanza kujidhihirisha ikiwamo kuongezeka kwa joto, mvua zisizotabirika, mafuriko na ukame.

Athari hizo zimeharibu maisha ya mamilioni ya watu na kuwaweka katika hatari zaidi ya kukabiliwa na njaa, kudhoofika kiafya na kusababisha migogoro kama vile ya wafugaji na wakulima wakigombea maji, ardhi ya kilimo au malisho ya wanyama wao.

Athari hizo pia hazijawaacha watoto ambao kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF), karibu kila mtoto duniani yuko hatarini kutokana na moja ya hatari zitokanazo mabadiliko ya hewa na mazingira kama mafuriko, joto, vimbuka, ukame na magonjwa ya kuambukizwa.

Februari mwaka jana, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anazindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 mjini Dodoma, inayosisitiza uhifadhi mazingira kwa kulenga kulinda vyanzo vya maji, misitu na upandaji miti.

Katika uzinduzi huo upandaji wa miti unatajwa kuwa endelevu ili kuibadili nchi iwe ya kijani kwa kurejesha hali ya asili ya mazingira iliyoharibika kutokana na shughuli mbalimbali na mabadiliko ya hali ya hewa moja ya changamoto inayorudisha nyuma utunzaji wa mazingira na kutokuwapo na elimu ya kutosha kuhusu dhana ya mazingira ikiwamo athari za mabadiliko ya hali ya hewa na namna ya kukabiliana nayo.

Kwa kuona umuhimu huo Taasisi ya Utu na Mazingira (HUDEFO), kupitia mradi 'Child Art Café' inatembelea klabu za mazingira kwenye shule za msingi na kufundisha wanafunzi namna ya kutunza mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa kupitia sanaa ya uigizaji na uchoraji.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Sarah Pima, anasema elimu hiyo wanaitoa kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la saba, ambapo huwafundisha somo moja kisha huwaongoza wachore au kulingana na walivyoelewa.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utu na Mazingira (HUDEFO) Sarah Pima, akitoa elimu ya utunzaji wa mazingira katika Shule ya Msingi Kibangu Ruge. **PICHA: JENIFER GILLA**

Anasema wanatumia sanaa hizo kwa sababu wanaamini kuwa mtoto anaelewa kwa njia ya vitendo hivyo somo hilo litakaa kwenye akili zao kwa muda mrefu.

"Somo la mazingira lina vitu vingi na vyenye mrengo wa kisayansi, kwa hiyo unapolipeleka kwa watoto unahitaji kutumia njia yenye burudani ili waelewe zaidi, ndio maana tunatumia sanaa ya uchoraji na maigizo au wakati mwingine nyimbo," anasema Sarah.

Mkurugenzi huyo anasema lengo la programu hiyo ni kuandaa vijana watakaoendeleza mapambano dhidi ya athari ya mabadiliko ya hali ya hewa kwa njia ya upandaji na utunzaji wa miti pia kuwapa fursa ya kutoa mchango wao juu ya namna kukabiliana na janga hilo.

"Samaki mkunje angali mbichi, ukiangalia vijana wa sasa wengi hawana mwamko wa kutunza mazingira kwa sababu hawakufundisha tangu wakiwa wadogo, programu hii inalenga kurekebisha makosa hayo, tunaandaa askari wa mazingira wa hapo baadaye waje waendeleze pale tutakapoishia," anasema Sarah.

Mratibu wa Mradi wa HUDEFO, Zainabu Mzirai, anasema mafunzo hayo pia yanaambatana na mashindano ya sanaa ya mazingira yatayokutanisha shule zote wanazozitembelea na mwishoni wa mwaka watamtangaza mshindi na kumpa zawadi.

Anasema mradi huo unashirikisha shule zote za serikali na binafsi na mpaka sasa wamezifikia shule sita na wanafunzi 30 kati ya shule 20 na wanafunzi 600 waliopanga kuwafikia mpaka mwishoni mwa mwaka huu.

"Mwishoni mwa mwaka huu tunatarajia kufanya maonyesho ya sanaa za mazingira kwa kuwashirikisha watoto na wazazi jijini Dar es Salaam, ambapo kazi ya wanafunzi hawa zitaonyeshwa na kushindanishwa mshindi atakabidhiwa zawadi, lengo ni kukuza hamasa kwa watoto kupenda utunzaji wa mazingira," anafafanua Zainab.

Anaongeza kuwa lengo la kuzifikia shule zote za msingi nchini, ikiwamo kuanzisha klabu za mazingira kwenye shule ambazo hazina ili kila mtoto apate nafasi ya kushirikiana katika kuboresha ustawi wa mazingira yake ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

James Bitisigirwe ni Mkuu wa Shule ya Msingi ya Kibangu inayonufaika na mradi huo, anasema kuwa wanaona fahari kufikiwa na shirika hilo kwa kuwa wanawaongezea ujuzi kwa namna ambayo wao hawawezi kufanya kutokana na uelewa wao.

"Mashirika kama HUDEFO anapokuja kufundisha watoto masuala ya mazingira tunajisikia furaha kwa sababu tunaamini watoto wenu watapata elimu zaidi, watu hawa wamebobea katika mazingira wanafahamu vitu vingi kuliko sisi," anafafanua James.

Anasema tangu kuanzishwa kwa klabu hiyo wamepata mafanikio makubwa ikiwamo wanafunzi kubadili mitazamo yao kuhusu mazingira na kuyachukulia kama ni kitu kinachohitaji kutunzwa na kuthaminiwa kwa manufaa ya baadaye.

"Mtoto aliye katika klabu ya mazingira akiona mti umenyauka unamuona anaonyesha kujali, atakufuata na kukwambia mwalimu ule mti unahitaji mbolea na maji maana unaelekea kufa, tofauti na mtoto ambaye hayupo kwenye klabu hiyo," anasema.

Alisema ukiacha klabu ya mazingira shule hiyo ina klabu nyingine nyingi ikiwamo haki za binadamu, kupika, kuchora na hisabati lengo ni kuwapa watoto nafasi ya kukutana nje ya darasa kujifunza na kujadili mambo mbalimbali ya kijamii yanayotendeka nje ya masomo ya darasani.

James anasema kuna faida kubwa za elimu ya ikolojia shuleni ikiwamo wanafunzi kujifunza kwa ushirikiano, kufikiri kwa makini na kufanya majadiliano na wengine.

Anasema pia wanafunzi hushiriki katika shughuli za kikundi ambazo huongeza uvumilivu na kuelewa uwezo wa kila mwanafunzi, ambazo ni sifa muhimu za uongozi.

Anasema klabu hizo pia zinasaidia kukuza vipaji vya watoto na kuwatambulisha kwenye shughuli za kijamii ili wanapokuwa wakubwa wajiendeleze na kufanya shughuli hizo.

"Kupitia klabu hizi wanafunzi huja na mikakati ya utekelezaji inayohusiana na matumizi ya ulimwengu halisi, hivyo kuboresha ujuzi wa kijamii na mazungumzo," anasema.

# Tanzania inapong'ara kilimo, chakula Afrika

**INATOKA UK.11**

kutengeneza nati, bolti, mashine na mitambo ya kilimo nao wapewe kipaumbele kwenye mradi wa sasa wa kilimo.

Ikumbukwe kuwa wataalamu wa 'agri mechanics' au zana za kilimo wanaeleza kuwa jembe la trekta au 'disc', 'haro', plau ya mkono ni mwendelezo wa utaalamu wa kuunda jembe la mkono hivyo ni mambo ambayo hayana tofauti, kinachoweza kuvitofautisha ni malighafi inayotumiwa, umbile(umbo) la kila kimojawapo, hivyo Tanzania haina sababu ya kuendelea kuwa mtumwa wa kuagiza vifaa hivyo ng'ambo ijizatiti kama China ilivyofanikiwa kubuni na kuhaulisha teknolojia yake, kwa vila hata Tanzania wasomi na wataalamu wa kilimo wapo.

Kwa kurejea kinachoendelea TEMDO inawezekana taasisi hiyo ikaunda majembe ya matrekta, haro, plau na kuachana na kuagiza vifaa hivyo kutoka nje miaka ijayo.

Pamoja na uwekezaji huo Tanzania inavyojipanga kuilisha Afrika na kuwa hifadhi ya chakula ya bara hilo inahitaji viwanda vya kutengeneza vifaa vya kilimo, umwagiliaji kwa nia ya kuwezesha kuzalisha vipuri vidogo lakini kwa lengo la kuunda mashine kamilifu au nzima zinazoweza kutumiwa kwenye kilimo kiasi miaka inavyokwenda.

Kama Tanzania imepanga na inataka kuendeleza sekta yoyote azima ya kwanza iwe pia kuwekeza kwenye teknolojia ya kuzalisha nyenzo zinazotengenezwa hapa nchini kama siyo zote angalau kwa kiwango kikubwa zaidi.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Njia tofauti kuunda maneno ya Kiswahili Kenya ikirahisisha, Tanzania ugumu ukizidi

WAKATI Kiswahili kinapewa nafasi zaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki na hata kwingine, kukua kwake katika kubadili maneno ya Kiingereza kuhusu teknolojia au fani nyingine kutaleta tofauti ndani ya nchi watumiaji wa lugha hizo.

Watumiaji na watafiti wa Kiswahili ni Tanzania na Kenya ambazo zinaanza kuwa na mielekeo tofauti katika kuunda maneno. Hata Zanzibar inaweza kujitegemea au hata kuendana na Kenya inachokifanya.

Moja ya maeneo muhimu kwenye kukua kwa lugha za kitaifa katika karne iliyopita ilikuwa kuingiza maneno ya kisayansi kwa njia ya kuunda au kubuni mengine mapya.

Kazi hiyo inahitaji mwelekeo wa kitaaluma ifanyike kwa njia gani, kama ni kutohoa neno la kitaaluma lililopo au la kawaida, kwa mfano kwa Kiingereza au kuunda jingine kama wataalamu wa Tanzania wanavyoita 'kusawiri', likidhi mahitaji ya kisayansi katika matumizi yake. Tatizo ni kwamba hukuna aliyeweka kanuni za kufuata.

Eneo moja la kanuni za kisayansi za kuunda neno ni kujali hisia ambayo linaweza kuleta, kwani hisia hiyo ikiwa chanya kwa matumizi tarajiwa, inakuwa rahisi kwa watumiaji wa jumla kulifahamu neno hilo na likawa sehemu ya lugha ya kawaida.

Kwa Tanzania na kwingineko Afrika Mashariki, hiyo ina maana ya kukubali maneno ya kawaida ya Kiingereza yatamkwe kwa Kiswahili na yatumike, kwa mfano neno technology kuwa teknolojia.

Mathalani, neno 'scrap metals' hutamkwa skrepa

'ambako tafsiri rasmi inayokubalika ni 'vyuma chakavu.' Ni rahisi kukubali tafsiri hiyo, kwa uwazi kihisia.

Ziko tafsiri ambazo uwazi wake kihisia, ambao ni muhimu kuyakinisha neno akilini, kuliondolea mashaka na hata urahisi wa kulikumbuka unakosekana.

Inakuwa ni tafsiri ya kujaribiwa kwa baadhi ya watu na rasmi kwa wengine, na ndivyo baadhi ya maneno yalivyo, na pale taasisi rasmi ya kuunda au kubuni maneno imetoa au imetohoa neno hilo litaanza kutumika kama tafsiri ya serikali.

Sasa pale Kiswahili kinapotumika nje ya Tanzania, tafsiri rasmi za kiimla ambazo hazina msingi katika hisia ya kulielewa neno zinatafutiwa mbadala, unaofaa.

Ndivyo unavyoweza kuelezea tofauti zinazoanza kuibuka kati ya Kenya na Tanzania katika kubadili, kutafsiri au kuunda maneno badala ya kutamka tu kwa Kiswahili neno la kitaaluma la Kiingereza, kwa mfano 'barcode.'

Barcodes au kwa Kiswahili cha Tanzania msimbo milia, cha Kenya mistari ya namba. **PICHA: MTANDAO**

Ni alama inayoundwa kielektroniki kwa namba na mistari ya wima inayoweza kusomeka kwenye mashine zinazo 'scan' bidhaa. Barcode inapachikwa kwenye bidhaa mbalimbali na inatumiwa kuudhibiti ubora, uchakachuaji na hata wizi na kuweka usalama kwenye mauzo.

Inaweza pia kuwa ni nembo ya kidijitali yenye alama ya mistari kadhaa ya wembamba na upana tofauti ambayo inaundwa kwa mpangilio ambako hakuna uwezekano wa alama hiyo kurudiwa na mweka nembo wa bidhaa nyingine. Kwa vile ni ya kutumika kimataifa katika kuuza bidhaa lazima iwe maalum.

Tofauti ya kubuni maneno ya kitaaluma ilijitokeza wakati wa midahalo ya redioni kuhusu matumizi ya dijitali kwa biashara za wanawake, mojawapo ya michango ikawa ni suala la kupata 'barcodes' kama utambulisho wa bidhaa katika maduka makubwa aua supermarkets, ndani na nje ya nchi.

Ikatokea kuna wajadili kutoka nchi tofauti wakigusia kuenea kwa matumizi ya nembo dijitali hizo, ambazo hapa nchini zimepewa jina la 'misimbo milia' au msimbo milia kama ni mmoja na Kenya zinaitwa 'namba mistari.'

Unaona wazi kuwa huwezi kupotea kujua nini kinachozungumziwa ukisikia kampuni imepata 'namba mistari' kwa ajili ya bidhaa zake, na si rahisi kujua nini kimekosekana iwapo itatoka taarifa kuwa korosho zilikwama kuuzwa kwa kukosa msimbo milia.

Unaelewa si kwa kulisoma hapo kwa jinsi lilivyotumika ila uwe unalifahamu kabla, ili uelewe.

Suala hapa ni kuwa endapo tofauti kama hii itajitokeza kwa maneno mengi ya Kiswahili yanayohitajika kuwasiliana labda kati ya wafanyabiashara wa DRC au Burundi na wa hapa, ni rahisi zaidi kutumia maneno yaliyoundwa Kenya kuliko Tanzania kwani neno la Kenya litakuwa rahisi kuingiza kwenye matumizi kuliko la Tanzania. Ni moja ya vielelezo kuwa 'huko tuendako' nchi za nje zitakuwa zinakuza misamiati kutoka Kenya hata kama mfumo rasmi wa kuunda maneno au 'usawiri kamusi' kwa lugha ya kitaaluma utaendelea kuwa na nguvu hapa nchini.

Unaweza kusema kuwa hapatakuwa na matokeo hasi ya aina yoyote kwa nguvu ya kuunda maneno hapa nchini ila kuyaeneza kwa watumiaji wengine wa Kiswahili itakuwa vigumu, siyo tu kwa maneno ya kitaaluma ila hata kwa tafsiri za maneno ya kawaida, ambayo labda baadhi yake yamezoeleka hata kwa watumiaji na wakufunzi wa Kiswahili katika nchi jirani.

Kwa mfano mtu anazungumzia maneno mapya au maalum katika eneo fulani, ayatambulishe kama 'istilahi' za pwani au muziki.

Licha ya kuwa neno 'istilahi' lipo katika matumizi ya kitaaluma tangu miaka ya 1970 kuelekea mwishoni, yaani kwa waliowahi kufuatilia kazi za Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) wakati huo, bado wasomi wanahitaji kujua maana yake.

Katika ingizo la Septemba 12 mwaka jana katika mtandao wa Wikipedia mwandishi anazungumzia neno hilo kuwa na maana ya neno au maneno msamiati 'yanayotumika katika uga fulani' maalum, unaweza ukawa uga wa kimichezo au kitabibu.

Ndiyo taabu ya kuunda maneno kwa 'mchongo' wa Kiarabu au lugha za kikabila za Bara badala ya kuyaunda kutoka katika Kiswahili cha kawaida.

'Faulo' ni neno la soka na kuiita 'istilahi' ya soka ni kifurushi cha wataalamu kinachowawezesha wao kuelewana wao kwa wao huku wakiwaacha watumiaji wa kawaida gizani.

Ndiyo maana bado wanatafuta 'istilahi' ni nini, tangu 1977 hadi leo.

Kwa upande wa pili, kubadili 'barcode' kuwa Kiswahili inatosha tu kuwa na 'namba mistari' lakini anatokea mtu anataka kutumia neno 'fimbo' kwa lugha anayoijua mwenyewe, au bakora ya kutembelea ya mzee kwa lugha kama hiyo, msimbo iwe ndiyo msingi wa neno jipya, kuchukua nafasi ya 'bar' ile mistari.

Halafu anaona 'barcode' inafanana na punda milia, hivyo anapata muungano wa kifimbo na milia, kuwa msimbomilia.

Katika maeneo mengi maneno ya awali katika Kiingereza yanatumiwa na wazungumzaji wa kawaida, ila baada ya BAKITA kusanifisha neno ipo nidhamu ya kiserikali kwa taasisi za elimu na kiutawala, au habari, kutumia neno lililosanifiwa.

Kwa mfano kila mahali watu wanaangalia mpira 'live' halafu linatoka neno 'mubashara' badala ya live. Hata barcodes zingezeweza kutumika hivyo bila kubadili chochote, ila BAKITA ina itikadi kuwa hakuna Mtanzania anayeongea Kiingereza kama lugha yake, na ni kukosa uzalendo kubaki na neno la Kiingereza badala ya Kiswahili.

Fikra hii ipo kwa upande fulani Kenya, hivyo hawakubakiza tu 'barcodes' na badala wake wakalitafsiri kwa njia rahisi zaidi, 'namba mistari.'

Yako maeneo ambako lugha au maneno ya kilugha (kikabila) yanalazimishiwa wazungumzaji wa Kiswahili, kwa mfano watu walianza kutumia king'amuzi kwa 'decoder' halafu BAKITA wanasanifu 'kisimbuzi,' yaani kama yule 'mbuzi' anayetumika kukuna nazi, kile 'kisu' chenye ncha za kukuna nazi.

Unaweza kujiuliza vile vile 'password' itafsiriwe vipi kama 'nywila' badala ya 'neno siri' au 'namba siri' kama baadhi wanavyotumia. Kiswahili rahisi inajulikana kama neno la kuthibitisha utambulisho iwe namba, herufi au alama mfano *#.

Kwa ujumla tafsiri hizi zinafanya Kiswahili kuwa lugha ya kikabila yenye maneno yake maalum ambayo si rahisi kuyaelewa ukiyasoma bila kuyajua kabla. Hali hiyo huweza kudumaza Kiswahili kwani watu wanachoka kumezeshwa maneno mapya ambayo hayana mantiki kihisia.

ELIMU

NA DK. FELICIAN B.KILAHAMA

# Kasi ndoa za jinsia moja ni kuiandaa dunia kuwa 'jangwa'

JANGA la ndoa za jinsi moja linaweza kufananishwa na kuigeuza dunia kuwa jangwa kwa kuwa jukumu la kuzaa na kuujaza ulimwengu analopewa mke na mume linatishiwa kukosa mwelekeo.

Ni kwa sababu mwanamume anakuwa na ndoa na mwanaume mwenzake kadhalika mwanamama naye anaoana na mwanamke mwenzake, jambo ambalo halikuwa mpango wa Mungu ambaye ndiye mkuu wa maumbile.

Wiki iliyopita makala hii iligusia mama au Hawa ama mwanamke alitwaliwa katika mwanamume, hivyo mwanamume atawaacha wazazi wake na kuambatana na mwanamke na watakuwa mwili mmoja.

Sasa taswira za mwanamume kumuoa mwanamume, vivyo na mwanamke naye kuolewa au kuoa mwanamke mwenzie zinatoka wapi? Kusema kweli hali hiyo inaweza kuwa ni kukengeuka na hata kuvunja msingi wa ndoa kama ulivyowekwa na Mungu wa kuishi mume na mke.

Ushoga unaweza kufananishwa na ushetani pengine uliopitiliza kiasi kwamba mume amwoe mume mwenzake au mwanawake waoane eti wawe mume na mke, mbona ni jambo linaloshangaza.

Kumbuka lipo onyo kuwa binadamu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa, shetani amejizatiti kuwaangamiza baadhi kwa kutumia dhana ya kupendana eti ni haki ya msingi kwa mashoga kufanya hivyo wakati ni uovu wa aina yake.



Tangu mwanzo wa dunia imekuwa ndoa ya mke na mume na si wanandoa wa jinsia moja. **PICHA: MTANDAO**

Wanaume mnafunga ndoa ili iweje? Eti ni kuishi pamoja kama wanandoa wengine, mume na mke hii ni hatari maana hata wanyama wa porini hawako hivyo, tujiulize wenye tabia hizo hupata nini hasa iwapo huo ni upendo kinyume na mapenzi ya Mungu?

Kuna faida kwa binadamu aliyeumbwa kwa mfano na sura yake Mungu kufanya matendo kama hayo ambayo pia huchangia kueneza magonjwa yasiyotibika kama saratani ya uume, njia ya haja kubwa, utumbo mpana na viungo vingine,

Bahati mbaya wapo watu wengine ambao wao siyo mashoga wanapigia debe ushoga mfano, kusema hadharani kuwa shoga ni binadamu hivyo wanahitaji faragha kama watu wengine ama kweli wajinga ndiyo waliwao.

Ni binadamu hatukatai lakini wamekengeuka haiwezekani mwanamume ujibadilishe jinsi yako ya kiume na kujifanya kuwa ni mwanamke wakati hayajawahi kuwa na maumbile halisi.

Huo ndiyo ukweli na siyo kinyume chake. Hata, wakifanya mabadiliko na kuweka jinsi ya kike bado ni mwanamume haijalishi umewekewa vichocheo au hormones za kike, ni kama kujikataa.

Imeeandikwa mwanamume atawaacha wazazi wake na kuambatana na mwanamke, hakuna ilipoandikwa tofauti na hivyo vivyo hivyo kwa mwanamke na mwanamke.

Ushoga kwa maana ya watu wa jinsia moja kuwa mume na mke ni kwenda kinyume na kusudio la Mwenyezi Mungu kwa binadamu washirika kazi za uumbaji akiagiza kuzaa na kuongezeka na kuijaza nchi.

Kimsingi matendo ya uhusiano wa jinsi moja hayana la zaidi isipokuwa ni nafsi zenye kuzingirwa na uovu katika ulimwengu wa roho'.

Hii ndiyo vita vya kiroho ambavyo watu wanatakiwa kupigana nayo hadi ushindi upatikane. Hapa tunahitaji nguvu ya Mungu pamoja na kutii na kunyenyekea ili aepushe na mambo kama haya yasiyokuwa na utukufu maana ni giza nene.

Ni tatizo kwani mataifa yaliyoendelea ndiyo chimbuko la aibu hii kwa binadamu. Kuendelea kwao ndiyo msingi wa haya yote ikiwamo kumuweka Mungu kando wakidhani kuwa na kila kitu ni ruhusa kwa watu kufanya wanavyotaka hata kama ni kinyume na mapenzi yake Muumba.

Kutokana na mtazamo huo hawajali mtu anafanya uovu gani hivyo wakafika mahali ushoga ukapewa hadhi sawa na walioana wa jinsia tofauti. Utawala unaweka katiba, sheria na sera zinazohalalisha ushoga.

Kadhalika, imetengenezwa bendera yake ambayo rangi zake zinashabiiana na rangi za upinde wa mvua.

Hatari zaidi ni pale hata baadhi ya madhehebu mathalani Anglikana, katika mafaifa hayo kushabikia na kuunga mkono uhusiano huo

madhebu ya dini yanafanya hivyo ili iweje? Tunajiuliza, hakika ni kufanya matendo ya kukufuru kwa kwenda kinyume na maadili ya kiroho.

Hata vijana wengi wamejikuta wameingia katika mkumbo huo kwa kutazama na kuiga masuala yasiyofaa yanayovyofanyika katika mataifa makubwa, tabia ambazo ni-kinyume na maadili ya Waafrika na Mtanzania.

Mfano, wanaovaa suruali au kaptula 'milegezo' maana yake nini? Ni dalili zisizofaa za 'kiushoga'.

Vile vile, mwanamke kuvaa suruali zinazowabana na kuonyesha maumbile ni dalili za uovu au kuna msukumo gani.

Baadhi yetu, wanashabikia na kutetea mambo haya kwa hoja kwamba ni haki za binadamu wakati wakijua kuwa siyo sawa maana ni kinyume na maadili na tabia njema.

Haki gani hizo wanaume au wanawake kujifanya mume na mke ni kukengeuka kwa hali ya juu katika historia ya binadamu.

Niwaombe viongozi wa madhehebu mbalimbali wasimame imara kupinga jambo hili lenye ukakasi kuingizwa katika masuala ya kiroho. Kadhalika, inashangaza kupindukia unapomwona aliyewekwa wakfu na mchunga kondoo wa Mungu anageuka kuwa shoga na kuendelea kutoa huduma kwa waumini wa dhehebu lake?

Je, kama kuna taratibu za wahusika kufunga ndoa inakuwaje mfano, masuala ya mahari, sheria za ndoa? Kama sikosei Sheria ya Ndoa Tanzania imejengeka kwenyemsingi wa mwanamume kuachana na wazazi wake na kuandamana na mwanamke hivyo wakafunga ndoa na kuanzisha familia mpya kama sehemu ya jamii.

Matakwa haya ya msingi hayaendani na ndoa za kishoga maana ni kuanzisha familia feki.

Ipo 'hoja' kuwa binadamu wote tumekosa mbele za Mungu hivyo wote tunatenda dhambi na hakuna aliye msafi mbele za Mola. Sawa, lakini kisiwe kigezo cha watu wa jinsia moja kujifanya 'mume' na 'mke' kinyume na maumbile.

Kuhalalisha uovu katika jamii ni hatari, tena ni dhambi ya uzinifu, uasherati, ulawiti maana haiingii akilini kusema wenye jinsia moja wamefanya dhambi hiyo lakini kwa mtazamo wa uongo maana kujifanya 'mume mke' au 'mkemume' wakati kimaumbile hayuko hivyo ni uongo na kweli haimo ndani ya wahusika.

Naomba serikali ngazi zote na vyama vya siasa suala hili lisihalalishwe kisera wala kisheria ili kulinda maadili ya taifa letu. Viongozi wetu wakemee 'ushoga' kwa nguvu zote na kwa moyo wa upoe wahusika washauriwe ili waachane na tabia hiyo mbaya na ovu kupindukia.

Taifa lisihalalishe uovu juu ya uovu kwa kisingizio kuwa hakuna aliye msafi isipokuwa Mungu mwenyewe. Waliozaliwa wakiwa wanaume wabaki kuwa wanaume kadhalika wanawake wabaki kuwa wanawake na tuweze kuendeleza vizazi kupitia taasisi ya ndoa na siyo kinyume cha hapo.

Ni Mungu mwenyewe aliyeanzisha muungano wa mwanamume na mwanamke au familia, hivyo, inatakiwa iheshimiwe sana na kila mtu.

Kinyume cha hapo ushoga ni kuikosesha ndoa halali heshima inayostahili sawasawa na makusudi ya Muumba.



# Serikali yatenga bilioni 8/- uboreshaji mazingira ya kazi

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, amesema katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetenga Shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa wauguzi na wakunga nchini ikiwamo kuwasomesha ili kuwaongezea ujuzi.

Dk. Mollel alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akifunga maadhimisho ya miaka 70 ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC).

Alisema serikali inatambua umuhimu wa wauguzi na wakunga katika sekta ya afya hivyo ipo haja na kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji kazi ili kuendelea kutoa huduma bora za afya katika maeneo mbalimbali.

"Takribani asilimia 60 ya watumishi waliopo katika sekta ya afya ni wauguzi na wakunga hivyo hatuna budi kuweka mazingira mazuri kwa kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kuboresha maslahi yao binafsi," alisema.

Aliwataka wauguzi na wakunga kufanya kazi kwa kuzingatia maadili, miongozo kanuni na sheria ili kutoa huduma bora kwa wananchi na kupunguza malalamiko.

"Pamoja na kuboresha mazingira ya kazi, lakini wauguzi na wakunga mnapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ili kuisaidia serikali kutoa huduma bora na kupunguza vifo vya mama na mtoto," alisema.

Kadhalika, aliwataka madaktari kufanya kazi kwa ushirikiano na watumishi wa kada ya uuguzi na ukunga ili kuleta tija na kuifikia azma ya serikali ya kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wake.

"Sisi madaktari tumekuwa watu wa kujiona ndiyo kila kitu bila kujua kuwa bila wauguzi na wakunga hatuwezi wauguzi wakisema ndiyo sisi Wizara ya Afya tutapiga hatua katika malengo tuliyojiwekea," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la TNMC, Prof. Lilian Mselle, alisema lengo la kuanzishwa kwa baraza hilo ni kusimamia utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

"Lengo la Baraza hili na uuguzi na ukunga kuanzishwa mwaka 1953 ilikuwa ni kusimamia maadili kwa kada hii ili wananchi wapate huduma bora za afya," alisema Prof. Mselle.

Hata hivyo, alisema baraza hilo limeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kinidhamu kwa wauguzi na wakunga ikiwamo kuwafutia leseni na kuwafuta kwenye daftari la usajili waliobainika kuwa na hatia.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza na vijana zaidi ya 700 kutoka mikoa yote nchini waliokusanyika Hombolo jijini Dodoma jana kwa ajili ya mafunzo ya kilimo biashara ambapo baada ya mafunzo ya miezi minne watagawiwa mashamba bure na yenye miundombinu yote ya umwagiliaji na serikali. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC aagiza halmashauri kubuni fursa sekta kilimo

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ameziagiza halmashauri kuhakikisha zinabuni fursa mbalimbali kwenye kilimo na biashara ili kuwainua wananchi kiuchumi ikiwamo kuongeza ukusanyaji mapato.

Senyamule aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), kilichoketi kwa ajili ya kujadili mambo mbalimbali, ikiwamo kukuza ukusanyaji mapato katika halmashauri zote mkoani hapa.

Alisema halmashauri nyingi zina maeneo, lakini hawatoi yapimwe, hivyo wanapaswa kushughulikia suala la upimaji maeneo ili kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza jambo ambalo litapanua wigo wa kuongeza kipato kwa wakazi wa eneo husika na taifa kwa ujumla.

"Halmashauri tusiwe na dhana ya kuwa Dodoma ni kame, hatuna chakula sio kweli, tunachopaswa ni kuwa wabunifu kwenye fursa za uwekezaji, ikiwamo kuzitangaza ili wawekezaji waone na kushawishika kuja kuwekeza," alisema Senyamule.

Alisema halmashauri ambazo hazijatenga maeneo ya kilimo zikatenge na kuchimba mabwawa ambayo yatasaidia kwenye shughuli mbalimbali za ukuzaji kilimo.

Senyamule aliwataka Wakurugenzi wa Halmashauri zote kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ili mkoa utimize vipaumbele walivyojipangia.

Hata hivyo aliwataka viongozi hao kwenda kuweka vivutio kwa wawekezaji ili wilaya ziongeze mapato yao ya kila siku kwa sababu fursa zinahitaji uwekezaji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, alisema ili kufikia malengo ya kuongeza makusanyo kwa wilaya za mkoa huo zinapaswa kudhibiti upotevu wa fedha.

Kadhalika, alisema kila halmashauri inapaswa kutumia ardhi waliokuwa nayo kwa ajili ya kutafuta fursa mbalimbali kutoka kwa wawekezaji wanaojitokeza kuwekeza.

Alisema kinachopaswa ni viongozi kushirikiana pamoja na wananchi wa eneo husika katika fursa zinazojitokeza ili kuwahamasisha.

# Viongozi kisiasa watakiwa kutetea maslahi watumishi wa umma

**Na Peter Mkwavila**, KONGWA

VIONGOZI wa kisiasa wametakiwa kuwa mstari wa mbele kulinda na kutetea maslahi ya watumishi wa umma waliopo kwenye maeneo yao ili kuchochea kasi ya maendeleo.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, White Mwanzalila, alipokuwa akizungumza na wadau wa elimu katika kikao cha mwaka cha wadau kilichofanyika wilayani Kongwa.

Mwanzalila alisema kuwa watumishi wa umma waliopo katika maeneo ya kiutawala, wapo kwa ajili ya kusaidia jamii katika nyanja mbalimbali za maendeleo na sio maadui kwa viongozi wa kuchaguliwa.

"Hawa watumishi ambao wameletwa kwenye maeneo yetu, wamekuja kutusaidia kuwaendeleza wananchi wetu na sisi wenyewe hawa sio maadui zetu," alisema.

Naye Ofisa Elimu Msingi Wilaya ya Kongwa, Margareth Temu, akiwasilisha taarifa ya tathmini ya hali ya ufaulu kwa shule za msingi na sekondari, alitaja vikwazo vinavyorudisha nyuma wanafunzi kufanya vizuri ni pamoja na upungufu wa walimu, ukosefu wa chakula shuleni, mwamko duni wa jamii, utoro, mmomonyoko wa maadili na miundombinu ya madarasa.

Alisema kuwa ili kupunguza vikwazo hivyo jamii inapaswa kutumia fursa mbalimbali zilizopo katika maeneo yao ikiwamo walimu wastaafu na wasio na ajira.

Mwenyekiti wa kamati ya huduma za jamii na Diwani wa Kata ya Sejeli, Chilingo Chimeledya, alisema bado kuna baadhi ya wazazi wana tabia ya kushawishi watoto wao kukataa masomo na ameahidi kuwa yeyote atakayebainika atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, aliwataka watumishi kudumisha upendo na kuwataka viongozi wa vijiji na kata kuwatembelea ili kubaini kero mbalimbali zinazowakabili.

"Kuna baadhi ya viongozi wa vijiji na vitongoji hawatembelei shule, yaani wao wanajua shule ni kitu kingine na wao ni kitu kingine. Tukifanya hivyo hatutafanikiwa," alisema Chimeledya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Dk. Omary Nkullo, alisema jamii inapaswa kushiriki kikamilifu kwenye kutatua kero zinazoikabili ikiwamo masuala ya elimu licha ya uwapo wa nguvu ya serikali.





# Ukosefu fedha wakwamisha utafiti wa zao la pareto

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

UKOSEFU wa fedha umesababisha utafiti wa zao la pareto nchini usifanyike kwa zaidi ya miaka 20 na kusababisha kudorora kwa uzalishaji wake.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mratibu wa zao la pareto nchini, Billesi Mzirano mbele ya Bodi ya Wakurugenzi wa zao hilo iliyotembelea mashamba ya mbegu kwenye Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini TARI, Kituo cha Uyole jijini hapo.

Alisema kukosekana kwa fedha kunadidimiza juhudi za uzalishaji wa pareto na kusababisha zao hilo kutozalishwa kwa wingi.

"Tunakiri kuwa kwa miaka 20 sasa hakuna utafiti wowote uliofanyika wa zao hili aidha kubuni mbegu mpya au mbinu za kuzalisha, wakulima wetu wamekuwa wakilima kwa mazoea na kupata mavuno kidogo," alisema Mzirano.

Akizungumzia suala hilo, Mkurugenzi wa Bodi ya Pareto nchini, Lucas Ayo, alisema serikali imeanza kufanyia kazi tatizo hilo na Sh. milioni 200 zimetolewa kwa ajili ya kufanya utafiti wa uzalishaji wa mbegu.

Alisema fedha hizo zitatolewa kwa vituo vyote vya utafiti nchini ambavyo vinatafiti zao hilo na lengo ni kubuni mbegu mpya ambayo itaendana na mabadiliko ya tabianchi.

Aliwaomba watafiti wa kilimo kutumia ujuzi wao kubuni mbegu mpya zitakuwa rafiki wa mazingira vilevile kuwashauri wakulima matumizi bora ya ardhi ili wapate mavuno mengi.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Pareto, Gideon Mapunda, alisema kwa mwaka wanazalisha tani 3200, lakini malengo yao msimu wa kilimo 2024/2025 wanatarajia kuzalisha tani 9,000 baada ya kupata mbegu mpya.

Mjumbe wa Bodi, Damas Lubuva, alisema miongoni mwa vikwazo vya uzalishaji wa zao hilo ni kukosekana kwa mbegu bora kwa wakulima.




Meneja Masoko na Mawasiliano wa GF Trucks & Equipment, Smart Deus (wa pili kushoto) na Ofisa Mauzo wa kampuni hiyo, Peter Willium, wakijadiliana jambo na viongozi wa Chama cha Wachimbaji Madini Mbeya (Mberema) wakati wa semina ya namna bora ya kutumia mitambo ya XCMG na magari ya FAW kwa wachimbaji iliyofanyika Chunya mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICGA WETU**

# Homera: Toeni elimu umuhimu wa uhifadhi maji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amezitaka sekta za maji kutoa elimu kwa wananchi umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi endelevu ya maji. Pia amesisitiza umuhimu wa wadau hao kutoa elimu ya sera ya maji kwa kuwa ndiyo mwongozo wa kutekeleza majukumu yao ya kumtua mama ndoo kichwani, suala ambalo ni ajenda ya serikali kwa sasa.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wadau wa sekta ya maji kwenye uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika mabwawa ya majitaka, Kata ya Kalobe.

Alisema sekta ya maji ina wadau wengi hivyo ni vyema wakashirikiana kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kutokana na dunia kwa sasa kukabiliwa na mabadiliko ya tabianchi.

Alisisitiza kuwa kwa sasa serikali imedhamiria kumtua mama ndoo kichwani na ni jukumu la wadau wa sekta ya maji kuwaeleza mipango hiyo ili kusaidia rasilimali hiyo inatunzwa.

"Nawaagiza UWSA, RUWASA na watu wa Bonde la Ziwa Rukwa nendeni kwa wananchi mwaeleze sera ya maji inasema nini, lakini mtoe elimu ya uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji ili wananchi watambue kuwa ni sehemu ya utunzaji wa mazingira hususani kwenye kipindi hiki tunachokabiliana na suala la mabadiliko ya tabianchi," alisema Homera.

Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (UWSA), Simon Bukuku, alisema katika maadhimisho ya Wiki ya Maji wamepanga kupanda miti 3,000 ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Alifanunua kuwa eneo la Kalobe walipanda miti 150 na wataendelea maeneo mbalimbali ya vyanzo ili kuendelea kutunza ikolojia na uoto wa asili kuzunguka maeneo hayo.

Mkazi wa Kalobe, Fadhil Matiko, alisema wataendelea kushirikiana na Mamlaka za Maji kutunza vyanzo ambavyo vinasaidia upatikanaji wa maji maeneo wanayoishi.

Aidha, aliwaomba viongozi wa Serikali za Mitaa kuendelea kusimamia sheria ndogo ambazo zitatumika kuwaadhibu wananchi watakaobainika kuharibu mazingira na vyanzo vya maji.

# Wenye ulemavu waomba muda urejeshaji mikopo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WATU wenye ulemavu mkoani hapo, wameiomba serikali kuongeza muda wa urejeshaji mikopo unaotolewa na halmashauri kwa madai kuwa kulingana na hali zao wanashindwa kufanya shughuli za uzalishaji mali kwa wakati uliopangwa kurejesha fedha.

Mwenyekiti wa Wenye Ulemavu Mkoa wa Mbeya, Jimmy Mwambepu, alitoa kauli juzi na kusema ufanyaji wa shughuli za kiuchumi kwa kundi hilo ni tofauti na wengine kutokana na hali zao wakiongezewa muda watatimiza malengo yao ya kiuchumi.

"Yule ambaye sio mlemavu anaweza kwenda kufunga mzigo wa biashara akarudi na kuuza kwa wakati tofauti na mlemavu ambaye akifunga mzigo wake wa biashara analazimika kutafuta watu wa kumsaidia mpaka ufike anajikuta ametumia muda na gharama nyingi kuwalipa wasaidizi," alisema Mwambepu na kuongeza;

Tunaishukuru serikali kwa miaka hii miwili ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wenye ulemavu wamewezeshwa kiuchumi ikiwamo mikopo, shughuli za kilimo pamoja na kupata eneo la kujenga ofisi ya wenye ulemavu jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa Chama cha Wenye Ulemavu Wilaya ya Mbeya, Damas Mwambeje, alisema serikali imewawezesha kiuchumi kwa sasa wigo wa mikopo umeongezeka kutoka kukopeshwa vikundi hadi mtu mmoja mmoja.

Aidha, watu wenye ulemavu wamepewa kipaumbele kwenye sekta ya afya, elimu na nyingine pamoja na uboreshaji wa miundombinu kwenye maeneo ya kutolea huduma za kijamii.

**Mwenyekiti wa Chama cha Wenye Ulemavu Wilaya ya Mbeya, Damas Mwambeje, alisema serikali imewawezesha kiuchumi kwa sasa wigo wa mikopo umeongezeka kutoka kukopeshwa vikundi hadi mtu mmoja mmoja.**





# Polisi yatoa tahadhari vitendo udhalilishaji mitandaoni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Kitengo cha Upelelezi wa Makosa ya Kimtandao kutoka Jeshi la Polisi Zanzibar, Issa Mohammed Salum, amesema vitendo vya udhalilishaji wa kimtandao vinazidi kushamiri na wanawake ndiyo waathirika wakubwa katika mitandao hiyo.

Aliyasema hayo juzi katika mkutano maalumu wa kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA- Zanzibar).

Alisema hali hiyo ya ukatili na udhalilishaji kupitia teknolojia ya kimtandao siyo nzuri kwa sababu watumiaji wengi wa mitandao ya kijamii hawajui sheria, kanuni na taratibu za matumizi salama ya kimtandao hiyo. Mkuu huyo alisema Jeshi la Polisi linaendelea kupambana kudhibiti matukio hayo ili kuhakikisha uwepo wa matumizi sahihi ya teknolojia. Alisema ni vigumu kuzuwia video au picha chafu kutosambaa katika mitandao kwa sababu mitandao hiyo inamilikiwa na watu nje ya nchi.

"Jamii itumie njia salama za mawasiliano ili sheria isije ikawakuta wamefanya jinai bila ya kujijua, tumia simu yako kwenye kujijengea uwezo wa kimaendeleo yako binafsi na taifa kwa ujumla kuliko kushajihisha au kuweka vitu vya jinai na ukajikuta sheria imekukuta kwenye mikono yako,"alisema.

Saluma alisema Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya Mwaka 2015 Kifungu cha 23 ni kosa kwa mtu yeyote haruhusiwi kuanzisha au kutuma mawasiliano ya kielektroniki kwenda kwa mtu yeyote kwa lengo la kulazimisha, kutisha, kunyanyasa au kusababisha maudhi ya kihisia kwa mtu mwingine.

Alisema sheria hiyo inaadhabu yake ambapo atakayekiuka kifungu hicho atakuwa ametenda kosa na atawajibika iwapo atatiwa hatiani kulipa faini ya shilingi milioni tano au kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela.

Aidha, aliwataka wananchi hasa wanawake kuacha kutuma taarifa zao au picha zao katika mitandao ya kijamii kwa sababu wahalifu huzitumia vibaya hali ambayo inachangia kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji mitandaoni.

Hakimu wa Mahakama Maalum ya Udhalilishaji Mkoa wa Mjini Magharib Unguja Vuga, Sara Omar Hafidh, aliwataka wananchi kutumia mitandao ya kijamii vizuri kwa ajili ya maendeleo.

Alisema wanawake ni waathirika wa udhalilishaji katika mitandao ya kijamii, hivyo ni vyema kuitumia katika kuleta matokeo chanya na siyo kuitumia kwa kuwaondoshea utu na heshima waliyonayo.

Mwenyekiti wa Bodi ya TAMWA-Zanzibar, Asha Abdi, alisema wazazi na walezi wanajukumu kubwa katika jamii katika kuwalinda watoto na udhalilishaji na kuacha muhali. Hata hivyo aliwataka wanasaikolojia kwenda kwa wananchi katika kuwasaidia kuwapa ushauri nasaha waathirika wa vitendo vya udhalilishaji kwa sababu huathirika kisaikolojia.

Mwenyekiti huyo pia aliitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kudhibiti mitandao ambayo inakwenda kinyume na maadili, kwa kuonesha taarifa chafu ambapo mitandao hiyo inachangia udhalilishaji wa kijinsia.

## Wanaoishi maeneo ya miradi watakiwa kuwa wastahimilivu

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wanaoishi katika maeneo ya miradi ya ujenzi wa barabara wametakiwa kuwa wastahimilivu wakati utekelezaji wa miradi hiyo ukiendelea.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, aliyasema hayo jana alipofanya ziara katika Barabara ya Mwanakwerekwe ili kujionea tatizo lililojitokeza ya kukatika kwa bomba la kupitishia majisafi na salama.

Waziri huyo alisema ni jambo la kawaida kutokea kwa tatizo la uharibifu wa miundombinu wakati wa ujenzi wa miradi lakini kupitia ziara hiyo tayari wameshatoa maelekezo ya kuitatua.

Pia, alieleza kwamba ili kuepuka tatizo kama hilo la kukatika kwa miundombinu ya maji watendaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) watakuwa ni sehemu ya timu ya mkandarasi ili kuonesha maeneo ambayo miundombinu hiyo ipo kwa lengo la kuepusha uharibifu kama huo.

Aidha, alisema miradi yote hiyo inayotekelezwa na serikali ina dhamira njema ya kuwaletea wananchi maendeleo sambamba na kuwatatulia changamoto za upatikanaji wa huduma bora.

Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "B" Unguja, Hamida Mussa Khamis, alisema ziara hiyo inakwenda kuondoa changamoto sambamba na kurahisisha mawasiliano ya barabara kuelekea katika Hospitali ya Wilaya.



Mkuu wa Kitengo cha Upelelezi wa Makosa ya kimtandao kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar, Issa Muhammed Salum, akitoa mada kuhusu udhalilishaji wa kimtandao katika mkutano wa Siku ya Wanawake Duniani ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar uliofanyika juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri ataja faida ya karafuu kiuchumi, kijamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame khamis, amesema karafuu ni miongoni mwa zao la biashara ambalo linaimarisha uchumi wa nchi katika kuleta kipato na ajira kwa watu wengi.

Amesema zao hilo linaitangaza Zanzibar katika maeneo mbalimbali duniani.

Aliyasema hayo juzi Mkoa wa Kaskazini Unguja, wakati wa uzinduzi wa ugawaji wa miche ya mikarafuu kwa mikoa yote ya Zanzibar. Waziri huyo alisema lengo la kuzindua ugawaji wa miche hiyo ni kuongeza uzalishaji kwa mkulima wa zao hilo na kuimarisha pato la taifa nchini.

Shamata alisema serikali itaendelea kuimarisha uchumi wake kupitia kilimo, hivyo ni vyema wakulima wahakikishe kua miche hiyo inatakiwa kutuzwa na kuekwa katika hali nzuri ili kuongeza tija katika kilimo chao.

Alifahamisha kuwa katika kuelekea msimu wa mvua za masika wakulima wanatakiwa kujiandaa kupanda miche hiyo ili mvua itakapoanza wawe wameshapanda kwasababu kuchelewa kupanda kutasababisha mvua chache na miche hiyo kufa.

"Niwaombe wakulima wote wanaojishughulisha na zao hili kuwa wachukue jitihada za kupanda miche haraka ili kupisha hasara isiyo ya lazima kwa kuwa zao la mikarafuu litawaongezea tija na familia zao," alisema.

Alisema serikali inaendeleza mikarafuu kwa mkulima na kuhakikisha inawahamasisha wakulima katika masuala ya uvunaji na kusaidia vitendea kazi pamoja na kuwapatia fursa za mikopo kwa ajili ya kuendeleza kilimo hicho.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Seif Shaaban Mwinyi, aliwataka maofisa wa kilimo kuwa na kumbukumbu za wakulima wanaopewa miche ili kufuatilia katika makuzi yake kwa vile serikali imekua ikitoa miche kila mwaka kwa lengo la kuwainua wakulima katika kuleta mafanikio na kujipatia kipato. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mohmoud, aliwataka wakulima kuitumia fursa hiyo na watakapopewa miche hiyo wahakikishe kuwa wanaipanda ili lengo liweze kufikiwa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**EVALINE J OLOMY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1392-0529** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NATTA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIG/RB/6800/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HADIJA HAMIS** anatangaza kupotea kwa **CHETI CHA CHUO CHA UALIMU DARAJA 'A'** chenye usajili namba E.533/13 kilichotolewa na CHUO CHA UALIMU MKWAWA mwaka 1988. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MS/RB/6502/03**

## KUPOTEA KWA VYETI



Ndugu **ZAITUNI MOHAMEDI ALLY** anatangaza kupotelewa na vyeti vyake ambavyo ni cha kidato cha nne chenye **Index No. S0907-0060** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ZINGIBARI SECONDARY SCHOOL mwaka 2009. Pia cheti cha Diploma **TPSC (NTA) LEVEL 6 chenye REG:DSS.01/16/TG.67** mwaka 2018. Certificate (NTA) LEVEL 5 chenye REG:DSS.01/16/TG.67 mwaka 2017. Certificate (NTA) LEVEL 4 chenye **REG:BTCSS.01/15/TG.76** mwaka 2016, pamoja na Certificate ya MDEA LEVEL I mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeviona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi. TAARIFA POLISI:**TAN/RB/258380/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ...........TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA...........Mkoa...TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na................66/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: NOOR MOHAMED WALLI JALALDIN**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: NOOR ALLY LEMA**

### TANGAZO

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 27 mwezi 3 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wamarehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

Imetolewa leoTarehe ....20... mwezi ...03...mwaka 2023

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 19/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HUSSEN RAMADHANI MSALA wa CHINANGALI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWANAHAMISI HUSSEN NYANGE**

### TANGAZO

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 31 Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 17 Mwezi 03 Mwaka 2023.

COURT SEAL

...............HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO-MJINI
DODOMA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABUBAKARI MOHAMED NGARAMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA LAND CRUISER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 146 AHS.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/TR /RB/178/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HAMAD RAMADHAN SEBOMEZA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 899 CSR.** Chassis namba **KEFE7TA0000524.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/473671/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SILVESTER PAULO LUBINZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 325 ATK** aina ya **TRUCK** yenye Rangi ya **MULTICOLOR.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **KAH/TR/RB/198/2023.**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI NO.08/2023**

**CLAUD BOAZI SANGA::::::::::::::MDAI**

**DHIDI YA**

**1.JOSEPH JACKSON NSEKEYA::::::::MDAIWA**
**2.ERICK BURTON MAHENGE:::::::::MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: JOSEPH JACKSON NSEKEYA NA ERICK BURTON MAHENGE**

Fahamu kwamba CLAUD BOAZI SANGA amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 27/03/2023,saa 2:00 asubuhi,mbele ya Mhe.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
**Kumbuka:**Msipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo ninyi kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 06/03/2023.

........................
**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**06/03/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**

**SHAURI LA MIRATHI NA.1/2023**

**MIRATHI YA MAREHEMU EDAH MASANGULA MWASOMBELO**

**DHIDI YA**

**ELIA AMBAKISYE JONGO..............MWOMBAJI**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi ya usimamizi wa mirathi mnamo tarehe 20/02/2023.Hivyo mtu yeyote mwenye pingamizi na usimamizi wa mirathi hiyo unaamriwa kufika mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 22/05/2023, saa 2:30 asubuhi bila kukosa.
Elewa kwamba ukikosa kufika siku hiyo shauri hilo litasikilizwa upande mmoja.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu pamoja na muhuri wa mahakama hii leo 20/02/2023.

..................
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**MBEYA**






TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Maandamano yarindima Kenya, Afrika Kusini

**Na Maulid Mmbaga**

MAANDAMANO yameshuhudiwa nchini Kenya na Afrika Kusini, huku polisi wa mataifa yote mawili wakifanya jitihada mbalimbali kuyazuia ikiwamo kurusha mabomu ya machozi kuwatawanya mamia ya waandamanaji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini, ilitoa wito kwa raia wa Tanzania wanaoishi nchini humo, kuchukua tahadhari na kuwa watulivu, kujiepusha kuhusika kwa namna yoyote katika tukio hilo.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya ndani na kimataifa, maandamano hayo yaliitishwa jana na Kiongozi mkuu wa upinzani nchini Kenya Raila Odinga kwa ajili ya kupinga gharama ya juu ya maisha na madai ya udanganyifu katika uchaguzi wa 2022 nchini humo.

**Shughuli za biashara zimefungwa hususani katikati mwa mji mkuu wa Nairobi kutokana na maandamano yanayoendelea.**

Ghasia zilishuhudiwa katika baadhi ya maeneo ya jiji kuu la Nairobi na mji wa Kisumu magharibi mwa Kenya, huku maofisa wa usalama wakikabiliana na waandamanaji kwa kuwafyatulia mabomu ya machozi ili kuwatawanya waandamanaji hao waliobeba mawe na kufunga barabara.

Pia ilidaiwa kuwa mtu mmoja alipigwa risasi na kufa katika maandamano hayo, huku takribani watu 22 wakikamatwa, wakiwamo wabunge wawili wa upinzani Opiyo Wandayi na Seneta wa Kilifi Stewart Madzayo ambaye ni kiongozi wa wachache katika bunge la Seneti.

Viongozi hawo ni miongoni mwa wengine wa Muungano wa Azimio ambao waliwaongoza wafuasi wao katika maandamano yaliyokuwa yakiendelea kote nchini Kenya.

Inaelezwa kuwa Odinga aliyeshindwa katika uchaguzi wa urais mwezi Agosti 2022, alitoa wito wa kuandamana kutoka wilaya kuu ya kibiashara kuelekea Ikulu ya Rais William Ruto ili kurejesha kile walichokitaja kuwa ushindi ulioporwa.

Maofisa wa polisi waliokuwa wamevaa mavazi ya kujihami na waliokuwa na vifaa vya kutuliza ghasia, waliwarushia mabomu ya machozi mamia ya waandamanaji ambao nao walirusha mawe katika mitaa huku wakiimba "Ruto lazima aondoke."

Taarifa za vyombo vya ndani zilisema maandamano ya wafuasi wa Chama cha Muungano wa Azimio yaliendelea kushika kasi katika sehemu tofauti nchini humo huku wafuasi wa muungano huo wakionekana kulalamikia hali ngumu ya maisha.

Naibu Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua, alisema biashara za Kenya zimepoteza Sh. bilioni mbili kutokana na maandamano hayo yaliyokuwa yakiendelea nchini humo.

Pia Gachagua, alitoa wito kwa viongozi wa Azimio kusitisha maandamano, akisema ghasia ni mbaya kwa uchumi na kwamba Wakenya wanahitaji kurudi kazini kufanya kazi.

"Shughuli za biashara zimefungwa hususani katikati mwa mji mkuu wa Nairobi kutokana na maandamano yanayoendelea," alisema.

Vile vile, inaelezwa kuwa katika kaunti ya Kakamega, pia wafuasi wa Raila walikusanyika asubuhi na kuanza kutembea barabarani kwa mshikamano na wenzao wa Nairobi na maeneo mengine ya nchini humo.

Taarifa zilisema maofisa wa polisi wa kupambana na ghasia walifanikiwa kurejesha hali ya utulivu mjini Kakamega kutokana na maandamano hayo yaliyositisha shughuli za kawaida zikiwamo za usafiri na biashara.

Aidha, inaelezwa kuwa licha ya ahadi za Rais Ruto za kupunguza gharama za maisha tangu alipochukua mamlaka Septemba 2022, mfumuko wa bei umeendelea kuwa juu katika taifa hilo lenye uchumi mkubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Februari, mfumuko wa bei ulipanda hadi asilimia 9.2 kwa mwaka kutoka 9.0 ukilinganisha na mwezi uliopita, licha ya kuwa ni kiwango cha chini kuliko matokeo ya mwezi Oktoba ambao mfumuko wa bei ulifikia asilimia 9.6.

Odinga alipinga matokeo ya uchaguzi katika Mahakama ya Juu mwaka jana, lakini Mahakama hiyo ilithibitisha ushindi wa Rais Ruto na kulishuhudiwa matukio machache ya vurugu ambayo yalitia doa uchaguzi wa mwaka 2007 na 2017.



Hali ilivyo katika mitaa nchini Kenya baada ya maandamano yaliyozuka jana. **PICHA: MTANDAO**

## Serikali yakaa meza moja na waasi Sudan

**JUBA,** Sudan Kusini

VIONGOZI wa serikali ya Sudan Kusini na wale wa makundi ya waasi, wamefanya mazungumzo ya kutafuta amani ya kudumu kwenye taifa hilo baada ya kuvunjika mwaka uliopita na kwamba yanafanyika chini ya uratibu wa ofisi ya Papa Francis mjini Roma, Italia.

Inaelezwa kuwa majadiliano hayo yalikuwa yamevunjika kabla ya ziara ya Papa Francis kwenye taifa hilo, huku mratibu wa mazungumzo hayo, Paolo Impagliazzo, akisema yatakuwa ni mwanzo mzuri kuelekea kupata maridhiano ya kitaifa.

"Ujumbe wangu kwa watu wa Sudan Kusini ni kwamba mazungumzo ya kisiasa ndio njia nzuri ya kumaliza mzozo ulioko," alisema Impagliazzo.

Kiongozi wa kundi la upinzani linalofahamika kama Real SPLM, Pagan Amum, alisema mazungumzo hayo ni muhimu kufanyika.

"Lengo ni kujadiliana cha kufanya, ni muhimu kujuwa kwamba njia ya kuongeza kipindi cha mpito kama ilivyokuwa kwa nyakati zingine hazikusaidia kitu," alisema Amum.

Jenerali Thomas Cirilo Swaka ni kiongozi wa waasi wa National Salvation Front, akibainisha kuwa wanaona viongozi walioko madarakani wanahusika pakubwa kwa machafuko yanayoshuhudiwa na mgawanyiko baina ya raia.

"Ni huzuni kwa kuwa nchi imepasuka, nchi yetu inaanguka, hivi sasa kuna vita tofauti nchini mwetu," alisema Swaka.

Aidha, awali mazungumzo hayo yalisitishwa mwezi Septemba 2021 na Rais Salva Kiir, kwa madai ya kuongezeka kwa mashambulio ya waasi nje ya jiji kuu la Juba. **RFI**



## Matokeo uchaguzi wabunge yaanza kutangazwa Nigeria

**ABUJA,** Nigeria

MATOKEO ya uchaguzi wa ugavana na wabunge uliofanyika mwishoni mwa juma lililopita nchini Nigeria, yameanza kutolewa huku gavana wa jiji la Lagos kupitia chama tawala, akifanikiwa kuchaguliwa tena katika uchaguzi uliogubikwa na vurugu pamoja na vitendo vya rushwa.

Kwa mujibu wa katiba ya Nigeria, magavana ni miongoni mwa viongozi wenye ushawishi, ambao husimamia ugavi wa bajeti za majimbo yao ambazo ni kubwa kuliko hata zile za baadhi ya nchi za Afrika.

Aidha uchaguzi wa Jumamosi, ulihusisha kuchagua magavana 28 na wabunge zaidi ya 900, na kwamba ulifanyika ikiwa ni wiki tatu zimepita tangu mgombea wa chama tawala cha APC, Bola Tinubu, atangazwe mshindi.

Uchaguzi wa ugavana kwenye jimbo la Lagos, ulikuwa unatazamwa kwa karibu, hasa baada ya aliyekuwa mgombea urais wa Chama cha Labour Peter Obi, kushinda idadi ya kura kwenye jimbo hilo dhidi ya Tinubu.

Inaelezwa kuwa zoezi hilo lilikuwa kipimo kingine kwa chama tawala ikiwa bado kina ushawishi kwa wananchi au la, licha ya kuwa idadi ya wapigakura haikuwa kubwa kama ile iliyoshuhudiwa wakati wa uchaguzi wa rais. **RFI**

## HABARI MICHEZO

# SIMBA, YANGA SC ZAAHIDI KUTOISHIA ROBO FAINALI

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu kongwe nchini Simba na Yanga kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali kwenye michuano ya kimataifa, zimeahidi kutoishia hatua hiyo kwani tayari zimeona kuna uwezekano wa kusonga mbele zaidi ya hapo kama zitaendelea kupambana.

Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi iliyopita kwa kuirarua Horoya ya Guinea mabao 7-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam huku Yanga ikifanya hivyo Jumapili kwenye Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuichapa US Monastir ya Tunisia mabao 2-0.

Timu zote mbili zimefanikiwa kutinga hatua hiyo zikiwa na mchezo mmoja mkononi wa ugenini, Simba ikitarajiwa kumaliza dhidi ya Raja Casablanca nchini Morocco wakati Yanga ikimaliza dhidi ya TP Mazembe nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

**Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said na Mwenyekiti wa Wanachama wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, wamesema timu zao zinaweza kuvuka hatua hii endapo wakiendelea kupambana kama walivyofanya kwe-nye hatua za makundi.**

"Mpira si jambo la kuelezewa sana zaidi ya vitendo, walio uwanjani wameona na kwenye televisheni wameona na waliokuwa kwenye redio wamesikia, timu imecheza mpira kwenye kiwango kizuri na tumepata ushindi, hakuna kingine, timu si ya mtu au mchezaji mmoja, kila mmoja amecheza kwa nafasi yake na kiwango chake, jambo kubwa ambalo ninalolisema tunawapongeza wachezaji wote kwa kutekeleza mipango au 'plani' ya kocha na ikafanikiwa.

"Tunakwenda kucheza mechi ya mwisho dhidi ya Raja Casablaca kwa ajili ya kupata matokeo mazuri pamoja na kwamba tumeshavuka hatua hii, lakini tutakwenda kuleta ushindani kwa sababu mpira si ushindi peke yake ila pia ni burudani kwa hiyo lazima tuwaburudishe Waafrika na watu wengine duniani ambao watakuwa wanaangalia mchezo huu, kwa hiyo wachezaji wetu watatakiwa kuwaonyesha kile kilichosababisha wafike hapo walipo na nina uhakika tukiendelea kuweka nguvu tunaweza kusonga mbele zaidi kwenye hatua hii tuliyofikia," alisema Mangungu.

Naye Injinia Hersi alisema Taifa limepata heshima kuwa na timu mbili za Tanzania kuingia kwa pamoja kwenye michuano ya kimataifa na kuiona ikichanja mbuga.

Aidha, aliihakikishia serikali, wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa timu hiyo haitoishia njiani kwani waliweka malengo ya kufanikiwa kwenye mashindano ya ndani na wamefanya hivyo na sasa wanaweka malengo ya kufanikiwa kimataifa na hawatoliangusha taifa.

"Nawashukuru sana Wanayanga kwa nguvu walioionyesha mpaka leo tumeweza kupata haya matokeo, safari bado haijaisha, tulikuwa na malengo, tulikuwa na malengo ya kuvuka makundi, tumevuka sasa leo tumeingia robo fainali waendelee kutusapoti, huwezi kujua, inaweza kuwa nusu fainali, fainali au ubingwa," alisema Hersi.

## MINOTI YA MAMA...




Nahodha na mshambuliaji wa Simba, John Bocco, akiwa amejitwisha kapu la magoli lililojazwa mamilioni ya Mama, Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya timu hiyo kuzawadiwa Sh. milioni 35, na mwakilishi wa Rais, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, kutokana na ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Horoya AC ya Guinea kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumamosi iliyopita. Rais Samia ameahidi Sh. milioni tano kwa kila goli linalofungwa na timu hiyo pamoja na Yanga kwenye Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## WAFF, TAFF kujadili soka la wanawake

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa katika soka la wenye ulemavu kwa upande wa wanaume, sasa Shirikisho la Soka kwa Watu wenye Ulemavu nchini (TAFF), liko mbioni kuanzisha mchezo huo kwa wanawake, imeelezwa.

Hatua hiyo imekuja baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Soka la Watu wenye Ulemavu la Dunia (WAFF), George Hermann, kudhuru nchini kwa ajili ya ziara ya siku mbili kumulika maendeleo ya mchezo huo na mpango wa kuanzishwa soka la wanawake kwa wenye ulemavu.

Hivi karibuni Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema wako katika mchakato wa kukutana na TAFF kwa ajili ya kufanya mikakati hiyo ikiwamo mchezo huo kuchezwa na wanawake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa TAFF, Peter Sarungi, alisema Mkurugenzi Mtendaji huyo, yuko nchini kwa ajili ya kujadiliana mambo mbalimbali ikiwamo kujenga na kukuza mahusiano baini ya shirikisho hilo na WAFF.

Alisema katika majadiliano hayo ni pamoja na kumulika miradi ya maendeleo ya soka kwa kuanzisha soka la wanawake wenye ulemavu, vijana na watoto walioko shuleni.

"Hivi karibuni Rais wa TFF, Karia alidokeza juu ya kuazisha soka la wanawake kwa watu mwenye ulemavu, ujio wa Hermann, hilo litakuwa sehemu ya majadiliano makubwa kwa sababu tuko katika mipango hiyo," alisema Sarungi.

Alisema mbali na kukutana na TFF pia mkurugenzi huyo atapata fursa ya kutembelea Shule za Sekondari Pugu, Salvation Army pamoja na viwanja vya JMK Park ikiwa sehemu ya kuhakikisha Tanzania wananufaika na mradi huo.



# Pamba FC yaisaka Ligi Kuu, JKT Tanzania yashikwa

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1990, Pamba FC, yenye masikani yake jijini Mwanza, juzi iliendelea azma yake ya kutaka kurejea Ligi Kuu, baada ya kuidungua Ndanda FC bao 1-0 kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara, huku vinara wa Ligi ya Championship, JKT Tanzania wakipunguzwa kasi kwa kufumuliwa mabao 2-1 dhidi ya Pan African ya Dar es Salaam.

Bao pekee la Pamba lilifungwa na Rogers Gabriel dakika ya tano tu ya mchezo na kudumu kwa dakika zote 85 zilizobaki.

Timu hiyo imeweka rekodi ya kucheza mechi tatu ugenini na kushinda zote, ikiruhusu bao moja tu, hivyo kuonekana msimu huu imedhamiria kurejea kwenye Ligi Kuu baada ya kuteremka katikati ya miaka ya 1990.

Kwa matokeo hayo, Pamba imefikisha pointi 44 ikiwa kwenye nafasi ya tatu, ikiendelea kupigana kutaka kurejea tena kwenye Ligi Kuu, ambapo ilikuwa ni timu ya kutisha katikati ya miaka ya 1980, hadi mwanzoni mwa 1990.

Wakati Pamba ikipigana kufa kupona, Mabingwa wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1982, Pan African, waliwachapa vinara wa ligi hiyo Maafande wa JKT Tanzania mabao 2-1, kwenye mechi kali iliyopigwa Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam.

Kipigo hicho kimewapunguza kasi maafande hao ambao mashabiki wa soka wameshawatabiria kurejea Ligi Kuu msimu ujao.

Pamoja na kupoteza, JKT Tanzania bado inaendelea kuongoza ikiwa na pointi 53, ikifuatiwa na Kitayosce ambayo juzi iliichapa Copco mabao 3-1, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, ikiwa na pointi 46, Pamba ikishika nafasi ya tatu.

Matokeo ya mechi zingine ni Mashujaa kuichapa Biashara United mabao 2-1, Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma na Mabingwa wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1988, African Sports ikapokea kipigo nyumbani, Uwanja wa Mkwakwani cha mabao 2-1 dhidi ya Mbeya Kwanza.

## ZISIKUPITE

### LUKAKU ATAKIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Inter Milan akitokea Chelsea. ***(Todo Fichajes)***

### MAGUIRE KUWEKWA SOKONI

KLABU ya Manchester United iko tayari kumuuza nahodha na beki wa kati wa England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 30 na mlinzi wa Sweden, Victor Lindelof, 28. ***(Football Insider)***

### MILNER MKATABA MPYA

KOCHA Jurgen Klopp ameitaka Liverpool kumpa kiungo mkongwe wa England, James Milner mwenye umri wa miaka 37 mkataba mpya. ***(Football Insider)***

### ONANA AWANIWA CHELSEA

CHELSEA ina nia ya kumnunua kipa wa Inter Milan na Cameroon, Andre Onana, mwenye umri wa miaka 26, katika msimu wa majira ya joto. ***(Inter-Live, via Fichajes)***

### BOEY ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inataka kumsajili beki wa kulia wa Galatasaray, Mfaransa Sacha Boey, 22. ***(Aksam)***

### REUS KUBAKI DORTMUND

KIUNGO mshambuliaji wa Ujerumani, Marco Reus mwenye umri wa miaka 33, anataka kusalia Borussia Dortmund, ambako ni nahodha hadi mwisho wa kipindi chake cha uchezaji. ***(Sky Germany)***

### DIAZ AWINDWA NEWCASTLE

CHELSEA na Newcastle zote zinamfuatilia mshambuliaji wa zamani wa Manchester City, Brahim Diaz. Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 23, kwa sasa yuko kwa mkopo kule AC Milan akitokea Real Madrid, lakini anaweza kupatikana mwishoni mwa msimu huu. ***(Sun)***

### MIN-JAE NA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kufufua nia yao ya kumnunua beki wa kati wa Napoli na Korea Kusini, Kim Min-jae mwenye umri wa miaka 26, msimu huu. ***(Football Insider)***

### ANTONIA ATAKIWA EVERTON

EVERTON itamnunua mshambuliaji wa West Ham kutoka Jamaica, Michail Antonio mwenye umri wa miaka 32 msimu wa majira ya joto, iwapo wataepuka kushuka daraja. ***(Sun)***

### KUDUS KUBAKI AJAX

KIUNGO wa kati wa Ghana, Mohammed Kudus mwenye umri wa miaka 22, anatumaini kubakia Ajax hadi mwisho wa msimu huu licha ya Manchester United, Arsenal na Liverpool kumtaka. ***(De Telegraaf, via 90min)***

### MASUAKU KUNUNULIWA

KLABU ya Besiktas inajiandaa kuanzisha kipengele cha kununua mkataba wao wa mkopo wa beki wa West Ham kutoka Congo, Arthur Masuaku mwenye umri wa miaka, 29. ***(Fanatik, via Inside Futbol)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# COURTOIS: MBIO ZA UBINGWA KWA REAL MADRID ZIMEISHA

**BARCELONA,** Hispania

THIBAUT Courtois amekiri kwamba nafasi ya Real Madrid kushinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, imetoweka baada ya Barcelona kushinda 2-1 kwenye mchezo wa El Clasico Jumapili na kuwaacha Madrid pointi 12 nyuma ya vinara hao.

**Madrid walianza kwa kuongoza mapema pale kwenye Dimba la Camp Nou kutokana na bao la kujifunga la Ronald Araujo.**

Sergi Roberto alisawazisha kabla ya muda wa mapumziko na wakati timu zote zikisukumana kutafuta bao la dakika za mwisho, Marco Asensio alikataliwa bao la kuotea kabla ya Franck Kessie kufunga katika muda wa nyongeza.

Matokeo hayo yanamaanisha kuwa Barca wako kileleni wakiwa na pointi 68 na wako tayari kutwaa taji lao la kwanza la ligi tangu mwaka 2019, huku Madrid wakiwa nyuma na pointi 56 huku zikiwa zimesalia mechi 12 ligi kufikia mwisho.

**●●● Tulitaka kupigana hadi mwisho, lakini sasa ni tofauti ya michezo minne, wanatakiwa...**

"Ndio, tunapaswa kuwa waaminifu," alisema Courtois akiiambia Movistar, alipoulizwa ikiwa mbio za ubingwa zimekamilika.

"Tulitaka kupigana hadi mwisho, lakini sasa ni tofauti ya michezo minne... Wanatakiwa kupoteza michezo minne, na sisi inatubidi kushinda yote. Hakuna lisilowezekana, lakini ni gumu sana."

Asensio aliyetokea benchi alidhani angeweka hai matumaini ya Madrid kutwaa ubingwa alipobadilisha pasi ya Dani Carvajal dakika ya 81 na kuwaweka wageni mbele, lakini bao hilo lilikataliwa na VAR, uamuzi uliomkasirisha kocha Carlo Ancelotti.

"Tulistahili kushinda," alisema Ancelotti akiiambia Movistar.

"Mchezo ulishinda. Halafu tuna mashaka na bao lililokataliwa... Unafikiri lilikuwa la kuotea? Lazima tukubali, lakini nina mashaka yangu. Hakuna uhakika. Tuna haki ya kuwa na mashaka. "

"Sijui, kwa uaminifu," Muitaliano huyo alisema.

"Nilifikiri kuwa kuotea kulikuwa wazi kabisa kwenye Kombe la Dunia, kwa kutumia teknolojia ya kuotea. Nina mashaka yangu. Ilibadilisha mchezo. Je, ilikuwa ni kuotea? Sina uhakika. Ikiwa VAR ina uhakika, ni sawa."

Umakini wa Madrid sasa utaelekezwa Copa del Rey -- ambapo watarejea Camp Nou kucheza na Barca katika mechi yao ya nusu fainali ya pili Aprili 5, mwaka huu na Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo watamenyana na Chelsea katika robo fainali mwezi ujao.


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 518,

MECHI KALI
DUNDEE FC
VERSUS
AYR UNITED
1 | 1.87
X | 3.54
2 | 3.59

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG: DHAMIRA IMETUPA USHINDI



**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amewamwagia sifa wachezaji wa Manchester United baada ya kutoka nyuma na kuwafunga Fulham waliokuwa tisa uwanjani mabao 3-1 katika robo fainali ya Kombe la FA.

'Mashetani Wekundu' hao walifika nusu fainali ya 31 iliyovunja rekodi, huku mabao mawili ya Bruno Fernandes na mkwaju wa Marcel Sabitzer yakiwapa ushindi baada ya kuwa nyuma kwa bao la kwanza la Aleksandar Mitrovic kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Mchezo huo uliingia kwenye machafuko baada ya mwamuzi Chris Kavanagh kuwapa wenyeji penalti dakika 18 kabla ya mchezo kumalizika.

Baada ya kushauriana na VAR, na kumlima kocha wa Fulham, Marco Silva kadi nyekundu kwa kumtolea lugha mbaya mwamuzi, Kavanagh, alimtoa Willian kwa kadi nyekundu kwa kuzuia shuti la Jadon Sancho kwenye mstari na Mitrovic akafuatia kwa kumsukuma mwamuzi.

United walitumia vema faida yao ya namba na kukata tiketi ya nusu fainali na watakutana na Brighton na Hove Albion katika Uwanja wa Wembley, ambako walitwaa taji la EFL kwa ushindi dhidi ya Newcastle United mwezi uliopita.



## Arteta aumiza kichwa majeruhi

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, hana uhakika kama Takehiro Tomiyasu, atarejea msimu huu kutokana na jeraha alilolipata, ingawa ana matumaini 'Washikabunduki' hao watapokea habari chanya zaidi kuhusu mlinzi, William Saliba.

Tomiyasu na Saliba wote walilazimika kutolewa nje baada ya kuumia katika mchezo wa mkondo wa pili wa hatua ya 16-bora wa Ligi ya Europa dhidi ya Sporting CP - ambapo vijana wa Arteta walipoteza kwa mikwaju ya penalti.

Wachezaji wote wawili hawakuwapo wakati Arsenal ilipopata uongozi wa pointi nane kwenye Ligi Kuu England Jumapili kwa kuwafunga mabao 4-1 Crystal Palace, wakati wapinzani wao kwenye mbio za ubingwa huo Manchester City walipokuwa kwenye jukumu la Kombe la FA.

Alipoulizwa baada ya ushindi huo ikiwa jeraha la goti la Tomiyasu linaweza kumfanya kuwa nje kwa muda wote wa kampeni, Arteta alisema: "Hatujui, ni wazi daktari anamtathmini.

"Tumekuwa na tathmini moja, wanahitaji kuwa na tathmini nyingine kesho (leo), lakini haionekani vizuri, hilo ni la uhakika.

Ripoti zimesema Saliba huenda akalazimika kujiondoa kwenye kikosi cha Ufaransa kwa ajili ya mechi zijazo za kufuzu Euro 2024 dhidi ya Uholanzi na Jamhuri ya Ireland, lakini Arteta anatumai anaweza kurejea mapema.

627,720

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/03/23 | 22:45 | Italy vs England | 2.76 | 3.25 | 2.63 |
| 02. 24/03/23 | 02:00 | La Equidad vs Chico | 2.52 | 2.90 | 2.80 |
| 03. 24/03/23 | 04:10 | America De Cali vs Junior Barranquilla | 2.21 | 3.14 | 3.35 |
| 04. 24/03/23 | 12:00 | Australia vs Ecuador | 2.69 | 3.17 | 2.69 |
| 05. 24/03/23 | 13:30 | Japan vs Uruguay | 2.85 | 3.23 | 2.50 |
| 06. 24/03/23 | 14:00 | South Korea vs Colombia | 3.02 | 3.13 | 2.44 |
| 07. 24/03/23 | 20:00 | Bulgaria vs Montenegro | 2.60 | 3.15 | 2.88 |
| 08. 24/03/23 | 20:00 | Denizlispor vs Boluspor | 2.77 | 3.23 | 2.28 |
| 09. 24.03/23 | 20:30 | Saint Brieuc vs Nancy | 2.68 | 2.95 | 2.68 |
| 10. 24/03/23 | 20:30 | Cholet vs FC Versailles 78 | 2.44 | 3.16 | 2.79 |
| 11. 24/03/23 | 20:30 | Paris 13 Atletico vs Bourg Peronnas | 2.67 | 2.98 | 2.67 |
| 12. 24/03/23 | 20:30 | Sedan vs Dunkerque | 2.43 | 3.11 | 2.85 |
| 13. 24/03/23 | 20:30 | Avranches vs Le Puy | 2.21 | 3.16 | 3.16 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 21/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:00 | 4449 | Barito Putera vs Persis Solo | 1.96 | 3.28 | 3.39 |
| 17:00 | 2387 | Sheffield United U23 vs Burnley U23 | 1.40 | 4.87 | 5.59 |
| 17:00 | 5273 | Colchester U21 vs Millwall U23 | 2.84 | 3.88 | 2.04 |
| 17:00 | 5836 | Coventry U23 vs Peterborough U21 | 3.05 | 4.03 | 1.91 |
| 17:30 | 2719 | Greifswalder FC vs Tennis Borussia Berlin | 1.23 | 5.40 | 9.55 |
| 20:00 | 2364 | Ishoej IF vs Naesby BK | 2.31 | 3.38 | 2.70 |
| 20:30 | 2918 | SV Heimstetten vs Buchbach | 2.65 | 3.38 | 2.34 |
| 20:45 | 3366 | Bayern Munich W vs Arsenal W | 1.98 | 3.42 | 3.31 |
| 21:00 | 2016 | Berliner Dynamo vs Viktoria Berlin | 1.88 | 3.47 | 3.58 |
| 21:00 | 2948 | Turbine Potsdam W vs 1. FC Koln W | 3.78 | 3.94 | 1.72 |
| 21:00 | 3380 | VSG Altglienicke vs Babelsberg | 1.53 | 3.93 | 5.18 |
| 21:00 | 3410 | DJK Ammerthal vs SC Eltersdorf | 3.94 | 3.83 | 1.71 |
| 21:00 | 3928 | TSV Kornburg vs 1. SC Feucht | 2.49 | 3.37 | 2.49 |
| 21:00 | 5061 | Hessen Kassel vs VfR Aalen | 2.03 | 3.20 | 3.00 |
| 21:30 | 3499 | FC Altona 93 vs TSV Buchholz | 1.24 | 5.20 | 7.00 |
| 21:30 | 3990 | Deportivo Espanol vs Justo Jose De Urquiza | 1.97 | 3.01 | 3.84 |
| 22:30 | 1140 | Goytre United vs Barry Town FC | 8.43 | 5.34 | 1.24 |
| 22:30 | 5063 | Abergavenny Town vs Llantwit Major | 4.06 | 3.85 | 1.65 |
| 22:45 | 1956 | Gainsborough vs Marine FC | 2.07 | 3.32 | 3.17 |
| 22:45 | 2011 | Loughgall vs Annagh Utd | 1.80 | 3.54 | 3.69 |
| 22:45 | 2085 | Alvechurch vs Barwell | 2.12 | 3.59 | 2.87 |
| 22:45 | 2253 | Harrow Borough vs Bracknell Town | 4.65 | 4.24 | 1.54 |
| 22:45 | 2550 | Welling vs Taunton Town | 2.16 | 3.30 | 2.99 |
| 22:45 | 2633 | Chesham Utd vs Plymouth Parkway | 2.04 | 3.53 | 3.06 |
| 22:45 | 2684 | Farsley Celtic vs Darlington | 2.85 | 3.31 | 2.24 |
| 22:45 | 2770 | Potters Bar Town vs Bognor Regis | 2.50 | 3.57 | 2.38 |
| 22:45 | 3125 | Crawley Town vs Doncaster | 2.38 | 3.21 | 2.72 |
| 22:45 | 3156 | Kings Lynn vs AFC Fylde | 2.11 | 3.36 | 3.05 |
| 22:45 | 3206 | Stratford Town vs Leiston | 2.89 | 3.57 | 2.11 |
| 22:45 | 3234 | Salisbury City vs Hayes Yeading United | 2.80 | 3.58 | 2.16 |
| 22:45 | 3287 | St.Albans vs Cheshunt | 1.65 | 3.72 | 4.44 |
| 22:45 | 3388 | Hanwell Town vs Poole Town | 2.79 | 3.47 | 2.20 |
| 22:45 | 3585 | Spennymoor Town vs Leamington | 1.99 | 3.33 | 3.38 |
| 22:45 | 3640 | Stirling vs Forfar Athletic | 1.81 | 3.43 | 3.74 |
| 22:45 | 3957 | Chippenham Town vs Weymouth | 2.11 | 3.36 | 3.05 |
| 22:45 | 4051 | Accrington vs Plymouth | 3.64 | 3.44 | 1.94 |
| 22:45 | 4144 | Metropolitan Police vs Swindon Supermarine | 2.50 | 3.68 | 2.34 |
| 22:45 | 4243 | Bromsgrove Rovers vs Rushden and Diamonds | 1.49 | 4.26 | 5.20 |
| 22:45 | 4788 | Gillingham vs Crewe | 1.70 | 3.42 | 4.57 |
| 22:45 | 4909 | Banbury United vs Curzon | 2.25 | 3.27 | 2.85 |
| 22:45 | 5155 | Bradford City vs Carlisle | 2.37 | 3.13 | 2.78 |
| 22:45 | 5315 | Lewes vs Canvey Island | 2.24 | 3.47 | 2.74 |
| 22:45 | 5547 | Marske United FC vs Liversedge | 2.09 | 3.78 | 2.80 |
| 22:45 | 5616 | Dundee FC vs Ayr United | 1.87 | 3.54 | 3.59 |
| 22:45 | 5880 | Farnborough Town vs Slough Town | 1.63 | 3.83 | 4.46 |
| 22:45 | 5945 | Albion Rovers vs Stranraer | 2.29 | 3.19 | 2.78 |
| 23:00 | 2262 | AS Roma W vs Barcelona W | 14.57 | 6.66 | 1.13 |
| 23:00 | 2612 | Institute vs Ballinamallard Utd | 2.34 | 3.33 | 2.62 |
| 23:00 | 5831 | Barnsley vs Sheffield Wed | 2.77 | 3.23 | 2.44 |
| 23:05 | 4986 | Los Andes vs Ituzaingo | 2.11 | 2.80 | 3.73 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# US MONASTIR, SINGIDA BIG STARS ZASAINI MKATABA WA USHIRIKIANO

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya US Monastir ya Tunisia imeingia mkataba wa kudumu wa ushirikiano na Timu ya Singida Big Stars kwa lengo la kusaidiana mambo mbalimbali ya uendeshaji wa klabu ikiwamo kwenda kuweka kambi nchini Tunisia kwa ajili ya msimu ujao.

**Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana baada ya utiaji saini mkataba huo, Mtendaji wa Klabu ya Singida Big Stars, John Kadutu, alisema mkataba huo utawasaidia kupata kiurahisi wachezaji kutoka Tunisia endapo kama watakuwa wanawahitaji pamoja na mambo mengine mengi ya kimaendeleo.**

"Mkataba huu utatusaidia sisi kupata wachezaji kiurahisi kutoka nchini Tunisia kwa ajili ya kuja kuitumika klabu yetu na endapo kama watamhitaji mchezaji wetu tutakaa na kuzungumza nao," alisema Kadutu.

Mtendaji huyo alisema maeneo ambayo watashirikiana na klabu hiyo ni kuisaidia timu yao ya vijana, sehemu ya kuweka kambi, utawala pamoja na kuwapa uzoefu wa kuendesha klabu.

Alisema amefurahi kufanya kazi na klabu kubwa kama hiyo na kudai walianza kufanya mazungumzo ya muda mrefu na uongozi wa klabu hiyo, kabla haijaja hapa nchini.

Kwa upande wa Rais wa Klabu ya US Monastir, Ahmed Belli, alisema mkataba huo utazinufaisha pande zote mbili na kudai wataendelea kushirikiana na timu nyingine Afrika, hasa ukizingatia timu yao ni miongoni mwa timu bora barani humu.

"Tunafurahia ushirikiano huu ambao una lengo la kunufaisha timu zote mbili kwa kusaidiana katika uzoefu wa uendeshaji wa klabu vile vile tuna timu nyingine kutoka Ivory Coast," alisema Belli.

Alisema wana timu kutoka nchini Ivory Coast ambayo wanashirikiana nayo kama walivyofanya kwa timu ya Singida Big Stars na kuweka wazi kuwa wana huduma nzuri ambazo zitawasaidia wachezaji kutimiza malengo yao.

Aidha, alisema ushirikiano huo utawapa nafasi wachezaji wa timu ya Singida kufahamika zaidi nje ya nchi kupitia klabu yao.

Klabu ya US Monastir ambayo ilicheza na Yanga juzi katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika na kufungwa mabao 2-0, ilianzishwa mwaka 1923 ambapo mpaka sasa imefikisha miaka 100.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Yanga imelipa kisasi kutokana na mchezo wa awali uliopigwa nchini Tunisia kukubali kichapo kama hicho.

Hata hivyo, timu hizo mbili zote zimefuzu robo fainali huku kila moja akibakiwa na mchezo mmoja mkononi, Yanga dhidi ya TP Mazembe ugenini na US Monastir ikiikaribisha nyumbani Real Bamako kuhitimisha hatua hiyo ya makundi.

## Rais kuipa Stars mil.500/-

INATOKA UKURASA 24

kumleta Kocha mpya, Adel Amrouche, yuko nchini Misri na tin inayojiandaa na mchezo wetu dhidi ya Uganda kuhakikisha tunapata ushindi katika mechi hiyo kabla ya kurudiana Machi 28, mwaka huu hapa nyumbani," alisema na aliongeza:

"Wachezaji wanatakiwa kupambana kuhakikisha tunafanikiwa kurejea na ushindi katika mchezo huo na ninamwagiza Naibu Waziri wangu, Hamis Mwinjuma (Mwana FA), kuongoza msafara na kwenda nchini humo kuongeza nguvu katika safu ya viongozi na wadau watakaokwenda nchini Misri," alisema Dk. Pindi.

Katika mechi hizo za kuwania kufuzu Afcon, Taifa Stars ipo Kundi F sambamba na Algeria, Niger na Uganda, ambapo timu mbili zitakazomaliza nafasi ya juu zitafuzu moja kwa moja kushiriki fainali hizo.

Algeria ndiyo inayoongoza kundi hilo ikiwa na pointi sita, ikifuatiwa na Niger yenye alama mbili huku Tanzania na Uganda zikifuata kutokana na kulingana kila kitu zikiwa na alama moja kila moja.




Rais wa Klabu ya US Monastir, Ahmed Belli (kushoto) na Mtendaji wa Klabu ya Singida Big Stars, John Kadutu, wakisaini mkataba wa ushirikiano kati ya klabu hizo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# *Mayele ni shida Yanga - Monastir*

INATOKA UKURASA 24

takiwa kupambana na kuheshimu mpira kwa ajili ya kusonga mbele, Tunaenda kucheza na TP Mazembe huku US Monastir wakimpokea Real Bamako nyumbani, tunatakiwa kupambana kupata pointi tatu ili tumalize kundi tukiwa juu," alisema Nabi.

Aidha, kocha huyo alisema alimtumia Ibrahim Abdallah (Bacca) kwa sababu ya uwezo wake wa kupiga mipira ya kichwa kwa kuwa US Monastir wanauwezo wa kucheza mipira juu, iliyokufa na kona kwa ufanisi mkubwa.

Kwa mara ya kwanza Bacca alipata nafasi ya kuanza kwenye kikosi cha kwanza cha Yanga katika mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya US Monastir ambapo alicheza sambamba na Bakari Mwamnyeto.

"Baka anakuja na kufanya vizuri siku hadi siku ndio maana ameingia katika kikosi kuna vitu anatakiwa kuongeza kwa sababu ya ukabaji wake," alisema Nabi aliongeza:

"Nawapongeza Simba pia kwa kutinga robo fainali hii ni ishara kubwa kwa mpira wa Tanzania, unakuwa na unapiga hatua kubwa na sasa ni muda wa kujipanga kwa mechi zijazo," alisema kocha huyo.

# Michezo

Jumanne Machi 21, 2023

Nipashe




'Mbio za ubingwa kwa Madrid zimeisha'

UKURASA 21

KILELENI TU...



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (aliyesokota nywele), akishangilia na wachezaji wenzake baada ya kuifungia timu yake bao la pili dhidi ya US Monastir kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# MAYELE NI SHIDA YANGA - MONASTIR

## Nabi yeye asema hesabu kumaliza kileleni, aigeukia TP Mazembe kwao...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa US Monastir ya Tunisia, Darko Novic, akiondoka na jina la Fiston Mayele, akidai ndiye aliyefanya mambo kuwaharibikia katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema kazi bado haijaisha kwani lengo lake ni kuona wanamaliza kileleni mwa msimamo wa Kundi D.

Yanga ikiwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya US Monastir kwenye mchezo wa hatua ya makundi wa Kombe la Shirikisho Afrika, hivyo kukaa kileleni mwa msimamo wa Kundi D kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa kutokana na kufikisha pointi 10 sawa na Watunisia hao.

**Akizungumzia mchezo huo Kocha wa US Monastir, Novic, alisema mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa na kwamba wachezaji walipambana, lakini haikuwa bahati kwao kupata matokeo.**

Alisema mchezo huo ulikuwa mgumu kwao kutokana na uwezo wa mshambuliaji wa Yanga, Mayele ambaye alifanya safu yake ya ulinzi kuwa na wakati mgumu katika kuhakikisha wanamchunga.

"Yanga ni timu nzuri, ina wachezaji wazuri ukizingatia wale wanaocheza pembeni, lakini kama nitapata nafasi ya kuchagua mchezaji mmoja kwenda naye robo fainali basi nitamchukua yule straika (Mayele)," alisema Novic.

Katika mchezo huo, Mayele alifunga bao la pili akimalizia pasi ya upendo ya Mzambia Kennedy Musonda ambaye licha ya kutoa asisti hiyo pia ndiye aliyetupia bao la kwanza nyavuni.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Yanga, Nabi yeye ameanza kupigia hesabu pointi tatu katika mchezo wa mwisho dhidi ya TP Mazembe, huku akisema lengo lao ni kuongoza kundi lao hadi mwisho.

Hii ni mara ya kwanza kwa Yanga kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho na mafanikio makubwa waliyokuwa nayo kwenye michuano hiyo ilikuwa ni kuishia hatua ya makundi tena ikimaliza mkiani mara mbili mwaka 2016 na 2018.

Nabi aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana dhidi ya US Monastir na kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali wakiwa na mchezo mmoja mkononi, lakini akasema bado hawajamaliza kazi.

Alisema mchezo ulikuwa wa ushindani mkubwa na ndani ya dakika 90 walitawala, hivyo wachezaji walifanya kitu kizuri kwa kupata ushindi huo uliowavusha na kusonga mbele kucheza robo fainali.

"Hatutaishia hapo tuna-

INAENDELEA UKURASA 23

## Rais Samia kuipa Stars mil. 500/- ikifuzu Afcon

**Na Saada Akida**

BAADA ya hamasa aliyoitoa kwa Klabu za Simba na Yanga kwenye michuano ya kimataifa kuendelea kuzaa matunda ya ushindi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, sasa ameigeukia Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars na kuiahidi mamilioni endapo itafuzu Fainali za Mataifa ya Afrika, Afcon 2023.

Rais Samia aliahidi na ameendelea kutekeleza kutoa Sh. milioni tano kwa kila goli litakalofungwa na Simba na Yanga kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika ambapo hadi sasa timu hizo zimeshalamba jumla ya Sh. milioni 85.

Simba inayopeperusha bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, imeshalamba milioni 45 huku Yanga yenye dhamana hiyo kwa upande wa Kombe la Shirikisho, ikiondoka na milioni 40.

Kupitia kwa Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Pindi Chana, Rais Samia ametoa ahadi ya Sh. milioni 500 kwa Taifa Stars, endapo ikifuzu kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika, Afcon 2023 ziakazofanyika nchini Ivory Coast.

Taifa Stars tayari imeshawasilini nchini Misri kujiandaa na mchezo dhidi ya Timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes) utakaopigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Ismailia, kabla ya timu hizo kurudiana Machi 28, mwaka huu katika Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana katika Ukumbi wa Benjamin Mkapa, Waziri Dk. Pindi, alisema Rais Samia anaendelea kutoa hamasa na ameahidi kutoa Sh. milioni 500 endapo Stars itafanikiwa kufuzu fainali hizo.

"Tayari serikali imefanikiwa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >